# Nipashe

Jumatano Mei 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581691

The Guardian digital

www.ippmedia.com **MWANGA WA JAMII**

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**RONALDO AVUNJA REKODI SAUDIA**

UK. 21

**Washtakiwa** 12 'lipa namba hii' kizimbani kisha 'selo' gerezani

UKURASA 4



**Waziri** aagiza uchunguzi ajali kiwanda Mtibwa ufanyike haraka

UKURASA 7



**Nishati** chafu ya kupikia inaua watu 32,000 kila mwaka nchini

UKURASA 5

# RPC kizimbani kwa kupinga mahakama

• **Ni** baada ya kuzuia dalali wa korti kutekeleza amri kukamata basi... *Endelea ukurasa 3*




**MAKONDA AWAKA...**

## Mkandarasi auza gari na nyumba yake kulipa madeni kisa DED

UKURASA 3

# UKIMWI wabainika chanzo kasi ya ongezeko la saratani

**Na Salome Kitomari**

ONGEZEKO la maradhi ya saratani limetajwa kuchochewa na watu wenye Virusi vya Ukimwi (VVU) na homa ya ini wengi wao kuacha kutumia dawa ipasavyo hali inayosababisha mashambulizi kwenye seli za mwili.

Aidha, ugonjwa wa kifua kikuu nao umetajwa kuwa tatizo kwenye jamii kutokana na kinga ya mwili kupungua kwa sababu ya mashambulizi kwenye seli.

UKURASA 2



**MICHEZO** **LOMALISA KUTUA AZAM FC** UK.23 **MAONI,** UK.6

# UKIMWI wabainika chanzo kasi ya ongezeko la saratani

**Na Salome Kitomari**

ONGEZEKO la maradhi ya saratani limetajwa kuchochewa na watu wenye Virusi vya Ukimwi (VVU) na homa ya ini wengi wao kuacha kutumia dawa ipasavyo hali inayosababisha mashambulizi kwenye seli za mwili.

Aidha, ugonjwa wa kifua kikuu nao umetajwa kuwa tatizo kwenye jamii kutokana na kinga ya mwili kupungua kwa sababu ya mashambulizi kwenye seli.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani (mapafu) na Mtafiti kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Elisha Osati, aliyasema hayo jana alipowasilisha mada ya hali ya Ukimwi nchini na utafiti uliofanyika katika nyanja mbalimbali kwa wahariri.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la AIDS Vaccine Advocacy Coalition (AVAC).

Alisema virusi vikiongezeka, uwezekano mkubwa wa mwenye maambukizi kupata saratani ni mkubwa huku akibainisha kuwa wakati wa UVIKO - 19 wenye virusi vya Ukimwi wengi walifariki dunia kutokana na mwili kupata mashambulizi.

Dk. Osati alisema kumekuwa na dhana mbaya kwenye jamii mtu anapotumia dawa kwa muda mrefu na kupunguza makali ya virusi kuwa chini ya 20 ambavyo havionekani kwenye vipimo, huona amepona na wengine kwenda kwa manabii kutoa ushuhuda kuwa wameombewa na kupona ugonjwa huo, hivyo kuacha dawa matokeo yake hali husababisha madhara makubwa baadaye.

Alisema utafiti unaonyesha mikoa inayoongoza kwa watu waliopimwa virusi kutoonekana na asilimia zake kwenye mabano ni Tanga (93.5), Njombe (86.7), Iringa (83.9), Mbeya (83.2), Songwe (87.2), Katavi (85.6) na Dar es Salaam (79.6).

"Hadi sasa haijulikani kilichochangia Tanga kuongoza ila kwa Njombe na Iringa kuna mashirika mengi ya kutoa elimu na kuna ufuatiliaji mkubwa wanaoishi na VVU kumeza dawa na kila mtoto anapozaliwa na mama mwenye maambukizi hufuatiliwa kwa karibu. Dar es Salaam kuna msaada mkubwa wa kutoa elimu na ilitarajiwa iongoze lakini ziko sababu zinazochochea hali hiyo," alisema.

Kuhusu lengo la kufikia 95-95-95 (malengo HIV isiwe ni ugonjwa mkubwa kwa madhara) ikiwa na maana asilimia 95 ya wenye HIV wawe wanajulikana, asilimia 95 wawe kwenye matibabu na asilimia 95 wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU, alisema utafiri unaonyesha kwa sasa wanaojulikana ni asilimia 82.2, walio kwenye matibabu asilimia 97.9 na wanaotumia dawa ni asilimia 94.3 huku wanawake wakiongoza kwenye makundi yote.

"Bado kuna kazi kubwa ya kufanya watu wapime, tuyafikie makundi hatarishi, hivyo lazima kuongea bidii. Katika wanaotumia dawa tumefanikiwa zaidi kwa sababu serikali ilibadilisha sera na sasa mgonjwa haangalii CD4 zake bali tumempima tumeona ana maambukizi anaanzishiwa dawa moja kwa moja. Pia unyanyapaa umepungua kwenye jamii watu hawajifichi," alisema.

Pia alisema taarifa zinaonyesha maambukizi mkoani Dodoma yaliongezeka kutokana na kasi ya watu kuhamia na kwamba ukuaji wa miji bila kuwa na tahadhari, maambukizi yanaendelea kuongezeka.

Dk. Osati ambaye ni Rais Mstaafu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MATI), alisema kipimo cha haraka cha HIV ni kizuri lakini hakipimi kwa kina hivyo wanaotaka kuanza mahusiano na waliopo wanapaswa kupima kwa kina ili kuwa salama.

Aidha, alisema kwa mujibu wa Tanzania HIV Impact Survey kwa mwaka 2023, Tanzania ilikuwa na maambukizi mapya 60,000 huku Zanzabar ikiwa na asilimia moja pekee na wastani wa hatua za kupunguza ni asilimia 78 na kwamba asilimia 4.4 ya Watanzania wanaishi na VVU.

**HOMA YA INI B**

Dk. Osati alisema homa ya ini B ni tatizo kubwa kwa sasa ambayo inaambukizwa na kufanya mapenzi bila kinga hali inayoongeza saratani ya ini, ini kusinyaa ambako husababisha kuvimba bandama ambayo husababisha mishipa ya koo na tumbo kuvimba kisha kupasuka na mgonjwa kutapika au kujisaidia damu.

"Chanjo ya homa ya ini inakusaidia sana kabla hujapata maambukizi ila ukishapata hakuna uwezekano wa kupona. Asilimia 95 ya wenye homa ya ini B hawaonyeshi madhara ila wanakuwa na usugu wa ugonjwa.

"Ni muhimu kupima kisha ukachanje, kuna watu wanabaki na ugonjwa bila madhara ila wanaambukiza wengine, kuna kiwango cha maambukizi kikifika mgonjwa anaanzishiwa dawa. Ukiwa na Homa ya Ini B hutakiwa kutumia pombe kali kwa kuwa unalipa ini kazi kubwa sana, linazidiwa.

"Tuna wagonjwa wengi kwa sasa hasa vijana tofauti na miaka ya nyuma tulizoea kuwaona wazee. Hadi mtu aonyeshe dalili za homa ya ini ni miaka 15 hadi 20 na wanafika kwenye hupima wakiwa katika hatua mbaya ini limeshambuliwa hadi kufikia asilimia 25.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la kutoa elimu ya afya linaloundwa na vijana, Dk. Lilian Mwakyosi, alisema ni muhimu kila mmoja akapima afya yake ili kuwalinda wengine na kuendelea kutoa elimu pamoja na kuweka afua mbalimbali ambazo zitaifikia jamii ngazi ya chini na makundi hatarishi.

Alisema kipimo cha njia ya mate (jipime) ni kwa ajili ya kuangalia viashiria vya uwepo wa Ukimwi mwilini lakini hakitoshi kuthibitisha kama mtu ameambukizwa au la na kwamba umuhimu wa kuthibitisha unasaidia kujua kama majibu mtu aliyoyaona yanaendana na hali yake.

# Makamba ataja vipaumbele vitano 2024/25

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imetaja vipaumbele vitano katika mwaka wa fedha 2024/25.

Moja ya vipaumbele hivyo ni kuratibu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ili kuchochea uwekezaji, utalii na biashara na kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa maendeleo ya nchi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alibainisha hayo jana bungeni wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2024/25.

Makamba alisema ili kufanikisha vipaumbele hivyo, aliliomba bunge kuidhinisha Sh. bilioni 241.09, kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 229.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 11.6 ni kwa ajili ya maendeleo.

Alisema katika kipindi hicho, wizara inapanga kuendelea kuimarisha uratibu wa ushirikiano wa uwili pamoja na ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa ili kulinda maslahi ya taifa na kustawisha diplomasia ya kisasa na kujenga uhusiano wa karibu na nchi washirika.

Kipaumbele kingine ni kuongeza ushawishi wa Tanzania kwa nchi zingine katika masuala mtambuka kwenye jumuiya na mashirika ya kikanda ya kimataifa.

"Kushiriki kwenye jitihada kikanda na kimataifa za kudumisha amani, ulinzi na usalama na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi, kuimarisha utawala bora na rasilimali watu pamoja na kutekeleza miradi ya ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi, makazi ya watumishi na vitega uchumi katika balozi za Tanzania na makao makuu," alisema.

Pia alisema wizara inajivunia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ikiwamo kuimarika kwa ushirikiano kati ya Tanzania na nchi zingine na taasisi za kimataifa.

"Mafanikio mengine ni upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, kuifungua nchi na kukuza biashara, uwekezaji, ufunguzi wa balozi mpya katika miji ya Vienna, Austria na Jakarta, Indonesia, kuongezeka kwa ushawishi na Tanzania katika majukwaa ya kikanda na kimataifa," alisema Makamba.

Pia alisema katika kipindi hicho, uteuzi wa Watanzania kwenye jumuiya za kimataifa umeongezeka, kuongezeka kwa ziara za viongozi wa nje nchini, UNESCO kutangaza Julai 7 ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani.

Kuhusu uratibu wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), alisema wana umuhimu mkubwa kutokana na mchango wao katika maendeleo ya Taifa.

"Mathalan, mwaka 2023, Diaspora wa Tanzania walituma Dola za Marekani milioni 751.6. Kwa kuzingatia umuhimu wao, serikali imejumuisha masuala ya Diaspora katika mapitio ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 na Sera Mpya ya Ardhi ya 2024 na kutoa hadhi maalum kwa raia wa nchi zingine wenye asili ya Tanzania ili kuwapa haki na upendeleo mahsusi," alisema.

Makamba alisema mwaka huu serikali itakamilisha kutoa hadhi maalumu kwa raia wa nchi zingine wenye asili ya Tanzania.

Alisema katika kutekeleza hilo, serikali itawasilisha katika Bunge mwezi ujao muswada wa mabadiliko ya sheria utakaokuwa na marekebisho madogo ya Sheria za Uhamiaji Sura ya 54 na Sheria ya Ardhi Sura ya 113," alisema.

"Aidha, niendelee kuwahamasisha diaspora wote kujiandikisha katika mfumo wa kidijitali wa kukusanya na kutunza taarifa ili watambuliwe na kunufaika na fursa mbalimbali," alisema Makamba.

Kuhusu ushiriki wa Tanzania kimataifa ikiwamo Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA) alisema umekuwa na manufaa makubwa wa Taifa.

Alisema Tanzania imechaguliwa kuhudumu kwa muhula wa pili katika nafasi ya ujumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha 2024 hadi 2026.

"Tanzania imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa Maadhimisho ya Miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika Mei, 2024, Tanzania kuwa mwenyeji wa Kongamano la Pili la Wanawake na Vijana katika Biashara kwenye Eneo Huru la Biashara la Afrika lililofanyika Desemba, 2023.

"Kupitishwa kwa Itifaki ya Wanawake na Vijana katika Biashara kwenye Eneo Huru la Biashara Barani Afrika ambapo Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kinara wa uhamasishaji wa wanawake na vijana katika biashara barani Afrika Februari, 2024," alisema.

Vile vile, alisema kampuni 11 za Tanzania zimeanza kufanya biashara chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, fursa za kutangaza na kuvutia uwekezaji katika Uchumi wa Buluu na kushirikiana na nchi wanachama wa jumuiya ya nchi za mwambao.

Hata hivyo, alisema dunia ya sasa ni ya ushindani wa nchi hushindania watalii, biashara, uwekezekaji, rasilimali za maendeleo, teknolojia na maarifa.

Alisema kushindana na kushinda katika zama hizi kunahitaji maarifa ya wanadiplomasia, rasilimali za kuwawezesha kutekeleza majukumu yao na ushawishi wa nchi kwa ujumla na kwamba Tanzania imejipanga kushindana na uwezo inao na maarifa inayo.

## HABARI KITAIFA

# Makonda amkalia kooni DED madeni makandarasi

**Na Beatrice Shayo,**
ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amemkalia kooni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Happiness Laizer, baada ya kushindwa kulipa madeni ya makandarasi.

Kutokana na hali hiyo, mkandarasi mmoja amesema ameugua ugonjwa wa moyo na kutokana na mali zake kuuzwa.

Kadhalika, Makonda amemtaka mkurugenzi huyo kuacha kuwalinda watumishi wake nane waliokula Sh milioni 52 na kuagiza wachukuliwe hatua.

Makonda aliyasema hayo juzi jioni wakati akiwasikiliza wananchi wa wilaya ya Monduli mkoani Arusha ambapo alishangazwa na kitendo cha mkurugenzi kutokulipa madeni ya wananchi hao huku akiendelea kuwalinda watumishi waliotafuna fedha za ushuru.

Awali, mmiliki wa kampuni ya ujenzi jijini Arusha, Julius Shelutete, alisema anaidai Halmashauri ya Wilaya ya Monduli Sh. milioni 144 kutokana na ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo aliyofanya bila kulipwa fedha.

Shelutete alisema amekuwa akifuatilia madai yake mpaka kwenye Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) bila mafanikio suala lililomsababishia kuugua ugonjwa wa moyo na kumlazimu kufanyiwa upasuaji kutokana na mali zake kuuzwa ili kulipa madeni.

Alisema kwa sasa amefilisika na mali zake kushikiliwa na kutaifishwa na kampuni mbalimbali kutokana na madeni yaliyotokana na zabuni alizokuwa akizifanya zilizokuwa zikimlazimu kuchukua vifaa vya ujenzi kwenye kampuni za saruji, nondo na vifaa vinginevyo vya ujenzi.

Shelutete alisema alijenga bweni la Shule ya Sekondari Kipoku na alitakiwa kulipwa Sh. milioni 69 na hakupatiwa na madarasa aliyojenga yaligharimu Sh. milioni 60 akalipwa Sh milioni 49.

"Nilijenga bweni la Mweta lenye vyumba vitano nikalipwa Sh milioni 18 ikabaki deni la Sh. milioni 45 mpaka sasa nalo sijalipwa," alisema.

Pia alisema Halmashauri ya Wilaya ya Monduli ilimpa zabuni ya kujenga jengo la zahanati ya Meserani na shule ya Meserani na tangu mwaka 2018 hajalipwa fedha yoyote licha ya ujenzi wa vyumba hivyo kukamilika.

"Nilichukua vifaa nikajenga zahanati ikafikia hatua ya kupaua Aprili, mwaka huu. mtendaji aliniambia zimekuja fedha Sh, milioni 400 nikaulizwa unadai Sh. ngapi nikawaambia Sh. milioni 19. Wakaniambia nitalipwa niendelee na ujenzi cha kushangaza hela imekuja sikupewa na kazi amepewa mtu mwingine kumalizia ujenzi," alisema huku akilia.

"Nimeshtakiwa na kampuni ya Tanga Cement nilichukua zaidi ya mifuko 800 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hiyo. Nimepelekwa mahakama ya Mwanza nimeuza fuso yangu kulipa hilo deni na bado nadaiwa. Mkurugenzi nimemwomba hata nipatiwe Sh. milioni 20 maana wamekuja wanataka kuuza nyumba wanayoishi watoto wangu," alisema.

Shelutete alisema fedha zinakuja na kazi anapewa mtu mwingine na akiuliza anaambiwa ni maelekezo kutoka kwa mkurugenzi na mpaka sasa ameshindwa kupata fedha zake ameandika zaidi ya barua 30.

Mkandarasi mwingine alimjulisha Makonda kuwa amejenga Shule ya Msingi ya Sokoine na anaidai halmshauri hiyo Sh. milioni 228 na tangu ilipokamilika mwaka 2007, amekuwa akizungushwa.

Alisema mwaka 2020 alipatiwa barua kutoka kwa Mkuu wa Mkoa Arusha na kujulishwa Halmashauri ya Monduli kutakiwa kulipa deni hilo kwa miezi miwili mpaka sasa akienda kufuatilia malipo hayo anapigwa danadana na tayari mali zake zimeuzwa ikiwamo nyumba ili kulipa madeni anayodaiwa.

Baada ya kusikiliza, alimtaka mkurugenzi kutoa majibu na kusema: "Ni kweli amekuwa akifuatilia madeni yake changamoto niliyokutana nayo ni madeni walikuwa wanakubalina na serikali ya kijiji."

Kutokana na majibu hayo, Makonda alihoji: "Nataka kujua mnamlipa lini? Mtu ameenda mpaka TAMISEMI, nataka uniambie hela yake mnamlipa lini? Mtu mpaka ameugua ugonjwa wa moyo kwa miaka mitatu na mali zake zinauzwa, miradi imefanyika. Kwa nini halipwi? Nipe majibu ya hela analipwa lini."

Makonda alimkatisha Mkurugenzi huyo baada ya kuona hatoi majibu ya kueleweka.

Awali, Makonda alimwambia Laizer kuwa kuna watumishi wanane wameondoka na Sh. milioni 52 za halmashauri kupitia 'pos' na kuhoji wako wapi na hatua gani zimechukuliwa.

Laizer alisema watumishi hao walitoka kwenye kikao na walipewa muda kwa ajili ya kuanza kulipa la sivyo watawachukulia hatua za kinidhamu.

"Mkuu wa Mkoa naomba unipe wiki moja ambayo tumekubaliana nao ili waweze kurejesha fedha hizo naomba kuwasilisha," alisema Laizer.

Baada ya majibu hayo, Makonda alihoji: "Mwananchi wa kawaida huwa hatua mnazichukua papo kwa papo tena wengine mnawatumia mgambo na polisi. Mwananchi huyo anapewa adhabu na hapewi muda lakini wanaokula fedha za umma iweje muwape muda?"

Mkurugenzi alijibu kuwa kuna mwingine kesi yake iko polisi na TAKUKURU kwa wale ambao walikuwa na fedha nyingi walipelekwa huko.

"Swali langu la pili Mkurugenzi mtu aliyekuwa anaiba fedha za wananchi amecheza na huu mtandao mpaka anachukua hizo fedha hapeleki, huyo adhabu yake ni kurudisha fedha. Kwa hiyo wanaishia kurudisha mbona wezi wengine wanafungwa. Utaratibu wenu ni kurudisha mkurugenzi naomba majibu fedha zetu ziko wapi" alihoji Makonda.

Mkurugenzi aliomba kulichukua jambo hilo na kukaa na vyombo vya dola ambavyo amewajulisha wadau hao ili wachukue hatua kwa pamoja kulipa fedha hizo.

"Hata hivyo, Makonda alihoji hatua za kinidhamu ni zipi anapobainika mtumishi ni mwizi?

"Hivi mwizi anaulizwa kwa nini asichukuliwe hatua za kinidhamu kwa hiyo mtumishi wizi wake una protocal mimi sikujua kama kuna itifaki ya wizi yaani wananchi wana utaratibu wao wa kushughulikiwa na wasomi wana utaratibu wao?"

Makonda alimtaka Mkurugenzi kutowafichia siri watumishi wake na kila mmoja anatakiwa kuwajibika katika nafasi yake.



# RPC abanwa kortini kuzuia kukamatwa basi lililoua

**Na Grace Gurisha**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Mtatiro Kitinkwi ameahidi mahakamani atatoa ushirikiano kukamatwa basi la Kampuni ya Mabasi ya Kilimanjaro lenye namba T 178 EAU, ambalo alitoa rukhsa liendelee na safari wakati lilikuwa limekamatwa na dalali wa mahakama.

Kitinkwi alifika juzi katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam baada ya kupata wito wa mahakama ili ajieleze kwanini alikiuka amri ya mahakama ya kukamatwa basi hilo lililotakiwa liuzwe ili familia ya Leonard Kisena ilipwe fidia baada ya kusababisha kifo cha Immaculate Kisena (16) aliyekuwa mwanafunzi wa kidato cha tano.

Msajili Sundi Fimbo wa mahakama hiyo, alimtaka kamanda wa polisi huyo ajieleze kwanini alifanya hivyo, naye alidai kuwa alipokea simu kutoka kwa abiria akilalamika kuzuiwa kuendelea na safari eneo la Shekilango, Dar es Salaam.

Alidai kuwa kibinadamu alitoa rukhsa waendelee na safari kwa sababu kupata basi lingine kwa wakati huo ilikuwa ngumu.

"Kwa sababu magari huwa yanakaguliwa kabla ya kuanza safari, nikaona kuruhusu gari lingine ambalo halijakaguliwa ingeleta shida, nikaruhusu liende halafu siku iliyokuwa inafuata (Mei 16, 2024) saa saba mchana basi hilo lipelekwe Kituo cha Polisi Oysterbay," alidai RPC Kitinkwi

Baada ya kueleza hayo, kamanda huyo aliahidi atatoa ushirikiano kukamatwa kwa basi hilo na kurudishwa kwa dalali wa mahakama ambaye ni Daniel Mbuga wa Legit Auction Mart.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Rolinda Sawaya alipoulizwa na mahakama kama alihusika kuzuia basi hilo, alidai kuwa hakuzuia na hajui mambo ya sheria.

Mkurugenzi huyo tangu shauri hilo lilipofunguliwa, hakuwahi kufika mahakamani hadi alipoandikiwa hati ya kukamatwa.

Baada ya hayo, Msajili Fimbo alitoa amri kuwa utekelezaji uendelee, magari yenye namba za usajili T 178 EAU na T 508 DDB yakamatwe na yakishakamatwa dalali awasilishe mrejesho mahakamani ili kupata ruhksa ya kuyauza. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Juni 3 mwaka huu.

Wakili wa Wadai hao, Mngumi Samadani, nje ya mahakama, alidai kuwa mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo baada ya kuwasilisha hoja mahakamani kutokana na dalali wa mahakama kuzuiwa kukamata gari wakati tayari mahakama ilishatoa amri.

Wadaiwa katika shauri hilo namba 47 la mwaka 2022 ni Kampuni ya Kilimanjaro Truck Ltd, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Rolinda Sawaya na Mjahidi Mohamed aliyekuwa dereva wa basi lililosababisha ajali lenye namba za usajili T 278 ALQ aina ya Scania.

Awali akisoma hukumu hiyo kwa niaba ya Jaji Leila Mgonya, Msajili wa Mahakama Kuu, Joseph Luambano alisema wadaiwa wote wanatakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 300 kwa kusababisha kifo, majeruhi na uharibifu wa gari.

Jaji huyo pia alisema watakapochelewesha malipo hayo watatakiwa kulipa riba ya asilimia saba kila siku kwa mwaka na pia wadaiwa watatakiwa kulipa gharama za kesi hiyo; haki ya rufani ipo wazi.

Kisena alifungua kesi hiyo ya madai namba 47, 2022 baada ya kupata ushindi katika Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani ambayo ilimtia hatiani Mjahidi katika kesi ya trafiki kwa kukiri kuendesha gari hilo bila kuwa na bima, kusababisha kifo, majeruhi Omenis Kabora na uharibifu wa gari aina ya Toyota Land Cruiser lenye namba za usajili T 323 CWB.

Kisena ambaye ni baba wa marehemu Immaculate, Desemba 24, 2021, akiwa na watoto wake wawili na mke wake walikuwa safarini kuelekea mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Alisema walipofika eneo la Kamala Bagamoyo saa 10:15 alfajiri, basi la Kilimanjaro liliacha njia na kuwagonga, ajali iliyosababisha kifo cha Immaculate papo hapo.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF AGRICULTURE**
**TANZANIA COTTON BOARD**

## ADVERTISEMENT FOR INTERNSHIP OPPORTUNITY

Tanzania Cotton Board is a statutory organization that was formed by the Act of Parliament No. 2 of 2001, and entrusted with the function of overseeing the growth and sustainability of the cotton sub-sector. Specifically, TCB deals with regulatory functions within the cotton sub-sector on behalf of the government which includes ensuring adherence to cotton farming procedures and regulations, ensuring steady supply of agro - inputs, maintaining a level playing ground for the cotton business companies and collecting, refining and disseminating information to the stakeholders.

Tanzania Cotton Board has some openings in the following positions that wants to be undertaken under INTERNSHIP basis.

**1. AGRICULTURAL OFFICER (Classification) (2 POSTS)**

**Duty Station: Shinyanga**
**Education Requirement:**
Holder of Bachelor Degree in any of the following: Agriculture General, Agronomy, Agricultural Engineering, Irrigation, Agro-mechanization or any other qualification from a recognised Institution.

**Duties and responsibilities:**
- To classify cotton in accordance with rules, regulations and International Standards.
- To conduct machine (HVI) calibration and sample testing
- To review, update and recommend any changes that may be for improvement of sampling instructions and classification techniques.
- To prepare and issue periodic reports on classification of cotton from various ginneries.
- To perform any other related duties as may be assigned by his/her Supervisor.

**2. ACCOUNTANT (2 POSTS)**

**Duty Station: Mwanza**
**Education Requirement**
Holder of Bachelor Degree or Advanced Diploma in one of the following fields: Accounting, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualifications from a recognized institution.

**Duties and responsibilities**
- To perform periodical cash accounting for each department to ascertain correctness of cash and book balances;
- To carry out examination of financial accounting and supporting documents;
- To evaluate the effectiveness of existing systems of internal control and recommend appropriate improvements; and
- To perform any other related duties as may be assigned by his/her Supervisor.

**3. PROCUREMENT OFFICER (1 POST)**

**Duty Station: Mwanza**
**Education requirement:**
Holder of Bachelor Degree in Materials Management, Procurement and Supplies Management, Logistics Management or equivalent qualification from a recognised Institution.

**Duties and responsibilities:**
- To assist in purchase or supply control of given lines of stocks;
- To assist in clearing and forwarding functions;
- To assist in record keeping for all procurement activities performed
- To support in implementing the functions of Tender Board;
- To assist in processing procurement tenders as per approved Authority's policies and procedures;
- To maintain register of approved suppliers for locally supplied items and updating it accordingly;
- To maintain register of all contracts and monitors supply of ordered goods;
- To assist in preparation of quarterly reports; and
- To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**4. STORES OFFICER (1 POST)**

**Duty Station: Mwanza**
**Education requirements:**
Holder of Bachelor Degree in any of the following field; Materials Management, Logistics Management or equivalent qualification from a recognized Institution.

**Duties and responsibilities:**
- To prepare bin cards and store ledger books;
- To assist in undertaking physical distribution;
- To maintain location index design;
- To carry out continuous stock checking and Annual Stock Taking;
- To assist in the preparations of quarterly reports;
- To assist in clearing and forwarding functions;
- To assist in keeping records and reports all procurement activities
- To prepare monthly stores report of all physical and card balances;
- To undertake stock review;
- To perform any other duties as may be assigned by his/her supervisor.

**5. PLANNING OFFICER (1 POST)**

**Duty Station: Mwanza**
**Education requirement:**
Holder of a Bachelor degree in any of the following fields: Economics or Agricultural Economics and Agribusiness or Statistics, or Project planning and Management Economics Planning or Planning and Investment or equivalent qualification from a recognized institution.

**Duties and responsibilities:**
- To assist in issues related to planning and budgeting;
- To assist in planning and control development projects;
- To assist in identifying income generation activities;
- To assist in the preparation of short- and long-term plan and strategies;
- To prepare guidelines for planning and assist in the coordination, preparation, implementation, monitoring and evaluation of the strategic plan;
- To perform any other related duties as may be assigned by his/her supervisor.

**GENERAL ELIGIBILITY CRITERIA FOR INTERNSHIP**
- Should be a Tanzanian Citizen;
- Should have acquired formal qualifications like a diploma, bachelor's degree or postgraduate degree from any recognized and reputable institution and have not yet been exposed to work experience related to their area of study;
- Should submit degree or academic transcript;
- Should have completed their studies within three years from the date of this advert;
- A commitment or desire of intern to follow a career in a specific occupation that has been identified;
- Only qualified candidates will be contacted for further processes;
- Application closing date will be 31st May, 2024.

**Mode of Application**
Application letters for those interested should be posted, e-mailed or hand delivered to the following address:

**DIRECTOR GENERAL**
**TANZANIA COTTON BOARD**
**REGIONAL DRIVE ROAD**
**P.O. BOX 61,**
**MWANZA.**
**E-mail: info@tcb.go.tz**



Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa mkutano uliowakutanisha maofisa uhamiaji wa Tanzania na Zambia, kujadili ushirikiano wa utendaji kazi kati ya nchi hizo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Uhamiaji wa Zambia, Dk. Japhet Lishomwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wapandishwa kizimbani kwa mashtaka utapeli mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Ifakara, mkoani Morogoro, Barnaba Gidajuri (45) na wenzake 11 wamepandishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka ya kuongoza genge la uhalifu na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu Sh. milioni 10.

Washtakiwa hao walipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ushindi Swalo.

Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, alidai mahakamani huko kuwa washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 32, likiwamo la kuongoza genge la uhalifu walilofanya kati ya Januari Mosi na Mei 5, 2024, wakidaiwa kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa simu kwa watu kisha kujipatia Sh. milioni 10.

Alidai kuwa katika shtaka ya pili na la tatu yanayomkabili mtuhumiwa Barnaba Gidajuri, yalitendwa Januari 4, mwaka huu, akidaiwa kusambaza ujumbe fupi kwa njia ya mtandao wenye maneno "Mzee huyu mganga wa tiba asili anatoa mali bila kafara, cheo, mapenzi...", "jiunge na chama huru cha freemason (666) Tanzania bila kutoa kafara ya binadamu..."

Mashtaka mengine manne yanayomkabili Barnaba. Inadaiwa kuwa akiwa Mkoa wa Morogoro, alitumia laini za simu zilizosajiliwa kwa majina tofauti bila rukhsa na idhini ya wamiliki.

Alidai kuwa mashtaka manane yanayomkabili mshitakiwa huyo alitenda Mei 11, 2024 kwa kujipatia Sh. 105,000 kutoka kwa Maria Nangwa baada ya kujitambulisha kuwa ni mganga atakayemtibu ugonjwa wake wa kifafa.

Katika shtaka la tisa na 10, Wakili Mafuru alidai yanamkabili Rahim Bangila (26), kwa kusambaza ujumbe mfupi kwa njia ya mtandao wenye maneno yanayosomeka "Mimi mwenye nyumba wako hapa, mbona siku zinazidi?"

Pia alidai mshtakiwa huyo anakabiliwa ni mashtaka matatu kwa kutumia laini za simu zilizosajiliwa kwa majina ya Valence Mandaki, Nundu Gulenya na Stephen Lihami bila rukhsa ya watu hao.

Wakili alidai mtuhumiwa mwingine Ramadhan Mcheni (28), anakabiliwa na mashtaka mengine mawili ya kutumia laini za simu zilizosajiliwa kwa majina ya watu wengine bila rukhsa yao.

Ilidaiwa mahakamani huko mashtaka mengine mawili yanamkabili Leonard Mwilenga (23) ambaye inadaiwa Mei 6 mwaka huu, alitumia laini za simu zilizosajiliwa kwa majina ya watu wengine bila rukhsa yao.

Wakili alidai mashtaka mawili mengine yanamkabili Mohamed Masalanga (24), ambaye alitumia laini ya Irene Said bila idhini yake.

Mashtaka mengine ni kusambaza ujumbe fupi kwa njia ya mtandao na kujipatia Sh. 389,000 kutoka Benki ya CRDB kwenda kwa Odilia Mathew kinyume cha sheria.

Alidai kuwa ujumbe huyo ulikuwa unasomeka "habari ya leo, mimi mwenye nyumba wako mbona kimya na siku zinaenda?" ...umepokea kiasi cha shilingi...". Pia anadaiwa kutumia laini yenye usajili wa mtu mwingine bila idhini.

Wakili alidai kuwa mashtaka mengine yanamkabili Noel Mboya (37) anayedaiwa kuharibu na kupoteza ushahidi kwa kuharibu simu aina ya Tecno na kupoteza uhalisia wa simu hiyo na kufanya ushahidi usionekane.

Wakili alidai mashtaka mengine yanayowakabili washtakiwa ni kujipatia Sh. milioni 10 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa watu mbalimbali kuwa fedha hizo zimetumwa kimakosa katika simu zao, hivyo zirudishwe.

Washtakiwa wote wanadaiwa kujipatia Sh. milioni 10 wakijua fedha hizo ni madharia ya mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Baada ya kusomewa mashtaka yao, washtakiwa hawakutakiwa kujibu kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri hilo. Washtakiwa walirudishwa rumande kutokana kesi yao kutokuwa na dhamana.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Juni 11 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wa kesi unaendelea.

# Nishati chafu yaua watu 32,000 kila mwaka nchini

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo amesema zaidi ya watu 32,000 hufariki dunia kila mwaka nchini kutokana na matumizi ya nishati chafu.

Vilevile, waziri huyo amesema kuwa kila mwaka nchi inapoteza zaidi ya hekta 469,420 za misitu kutokana na uharibifu unaochangiwa na ukataji kiti kwa ajili ya kupata nishati chafu ya kupikia.

Waziri huyo aliyasema hayo juzi mkaoni Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu wiki ya maadhimisho ya kitaifa ya mazingira duniani itakayoanza Mei 29 na kutamatika Juni 6 mwaka huu.

Dk. Jafo alisema matarajio ya serikali mpaka kufikia mwaka 2034, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Alisema matumizi ya nishati hiyo ni ajenda mahususi ambayo imechukua nafasi kubwa katika sera, mipango na mikakati ya serikali mbalimbali duniani.

Alitaja shughuli zitakazofanyika katika maadhimisho hayo zitajumuisha kutoa taswira kwa vyombo vya habari kuelekea Wiki ya Mazingira na uzinduzi wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa chini ya mradi wa urejeshaji uoto wa asili ambayo yeye anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

"Mei 31 mwaka huu kutakuwa na kongamano la kitaifa la wadau wa mazingira litakalokuwa na kaulimbiu ya 'Mabadiliko ya Tabianchi na Athari Zake', mgeni rasmi atakuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

"Siku itakayofuata kutakuwa na kampeni ya usafi wa mazingira kitaifa itakayofanyika Dar es Salaam, eneo la Coco Beach. Mgeni rasmi atakuwa Makamu wa Rais, Dk. Mpango, Kanda ya Ziwa Geita, mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa," alisema Jafo.

Alisema kwa Kanda ya Kati Dodoma, mgeni rasmi atakuwa Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, Nyanda za Juu Kusini Mbeya, mgeni rasmi atakuwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na kwa Kanda ya Magharibi Kigoma atakuwa mkuu wa mkoa huo.

Kanda ya Kaskazini Arusha, Dk. Jafo alsiema mgeni rasmi atakwua Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma na Kanda ya Kusini Lindi, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa mkuu wa mkoa huo.

Waziri Jafo pia aliomba wananchi kujitokeza kushirikiana na serikali katika maadhimisho hayo yenye kaulimbiu ya 'Urejeshwaji ardhi, Ustahimilivu na Hali ya Jangwa na Ukame'.

# Jela miaka 90 kwa kunajisi watoto

**Na Khadiha Kitwana,**
KILOMBERO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kilombero imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 90 gerezani Leonce Matea (55), mkulima na mkazi wa Chicago A', Kata ya Kidatu, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro baada ya kupatikana na hatia ya kunajisi watoto watatu.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mahakamani huko na Hakimu Bestina Saning'o baada ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mkaguzi wa Polisi Thomas Kamsini kuomba kutolewe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa hiyo ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo za kunajisi watoto.

Mshtakiwa Matea aliomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa umri wake ni mkubwa.

Hakimu Saning'o baada ya kusikiliza maombi ya kila upande, alimtia hatia mshtakiwa huyo na kumhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kila kosa aliloshtakiwa kwalo.

Hakimu Saning'o alisema kuwa ili iwe fundisho kwake na wengine, mahakama imemtia hatiana mshtakiwa katika mashtaka yote matatu ya kubaka na kila kosa atatumikia kifungo cha miaka 30, lakini adhabu hizo zinatekelezwa pamoja.

Baada ya kusomwa kwa hukumun hiyo na Hakimu Saning'o, Matea alichukuliwa na kupelekwa katika Gereza la Kiberege.

Novemba 24, 2023, Matea alifikishwa mahakamani huko na kusomewa mashtaka matatu ya kunajisi.

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa kuwa kati ya Juni Mosi, 2023 na Novemba 16, 2023, katika Kijiji cha Chikago, Kata ya Kidatu, Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro, alinajisi mtoto wa miaka tisa (jina limehifadhiwa).

Katika shtaka la pili, tarehe hizohizo na eneo lilelile, Matea anadaiwa kunajisi mtoto mwenye umri wa miaka 10 (jina limehifadhiwa).

Na katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa kati ya Novemba Mosi, 2024 na Novemba 16, 2023 , Matea alinajisi mtoto mwenye umri wa miaka mitano (jina limehifadhiwa).

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Matea alikana kutenda makosa hayo. Upande wa Jamhuri ulipeleka mashahidi 12 wakiwamo na waathirika wa shauri hilo.

Hata hivyo, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, inaelekeza adhabu ya kifungo cha maisha gerezani kwa anayepatikana na hatia ya kunajisi mtoto mwenye umri chini ya miaka 10.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi katika Barabara ya Uhuru, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri Silaa afunga ofisi ya Masjala ya Ardhi Dodoma

**Na Waandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amefunga Masjala ya Ardhi ya Jiji la Dodoma ikiwa ni hatua ya wizara yake kuondoa changamoto za sekta ya ardhi jijini.

"Tumeamua kufunga masjala hii ya jiji, nimetoka kuweka makufuli, tumeifunga. Tunahamisha shughuli hizi za ardhi kutoka hapa kuja ofisini kwangu kwa Waziri wa Ardhi.

"Na shughuli hizi tumezitoa hapa kwa sababu huyu aliyenyoosha mkono wa mwaka 2017 nikimpa nafasi aelezee mimi ninakosa majibu kama waziri mwenye dhamana ya ardhi," alisema waziri huyo alipozungumza na wananchi baada ya kufunga masjala ya ofisi hiyo jana.

Silaa alimwelekeza Katibu Mkuu wa wizara hiyo kusimamia shughuli hiyo ili kuhakikisha watu wanapata haki zao.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassab ametuelekeza tusimamie haki za watu wake na kazi hiyo tutaifanya kwa uadilifu mkubwa na ukisoma vitabu vyote vya dini vinaelezea kazi ya haki ni kazi ya Mungu," alisema Silaa.

Aliwaambia wananchi waliokwenda kupata huduma wakati wa kufunga ofisi hizo za Masjala ya Ardhi ya Jiji la Dodoma kuwa, ofisi za ardhi sasa zitafunguliwa rasmi siku ya Jumatatu tarehe 3 Juni 2024 kweye ofisi za ardhi ilipokuwa ofisi za Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema wizara yake itajenga ofisi ya kisasa yenye kamera zenye uwezo wa kuchukua sauti itakayosimamiwa moja kwa moja na ofisi ya waziri pamoja na Katibu Mkuu sambamba na kuweka maofisa waadilifu.

"Ninakwenda kujenga ofisi ya kisasa, itakuwa na jicho langu moja kwa moja, tutaweka maofisa waadilifu, binadamu wa siku hizi siyo binadamu wa zamani, tutaweka kamera ambazo zitachukua picha na sauti na wakati nikiwa Dar es Salaam na jimboni katika ziara nina uwezo wa kuingia kwenye simu yangu kuangalia Ofisi za Ardhi Dodoma wanafanya nini," alisema Silaa.

Kwa mujibu wa Waziri Silaa, mwelekeo wa Wizara ya Ardhi ni kujenga ofisi za kisasa ambazo wananchi watakuwa wakipata huduma kwa wakati mmoja.

Awali akizungumza na watumishi wa ardhi katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Waziri Silaa aliwataka watumishi hao kuwajibika wakati wa kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kila siku ya kuhudumia wananchi kwenye sekta ya ardhi.

Naye Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda alielekeza watumishi hao wa sekta ya ardhi kuwa tayari na kupokea mabadiliko yenye utendaji kazi wenye tija yatakayoleta uhai katika maisha ya watu.

"Daima lazima akili yako ihisi kwamba mabadiliko yoyote kwako ni darasa," alisema Naibu Waziri Pinda.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Makonda kuhusu wavivu, wazembe mwafaka

**MKUU** wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, hivi sasa yuko katika ziara ya siku sita katika wilaya za mkoa huo kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa pamoja na kusikiliza kero zinazowakabili wananchi katika masuala mbalimbali.

Ziara hiyo inafanyika wakati kiongozi huyo ameshakutana na wananchi wa makundi mbalimbali jijini Arusha na kuibua masuala mbalimbali kuhusu kero za wananchi ikiwamo wananchi kudhulumiwa na kuporwa mali zao. Pia alikutana na hadithi za watu kufanya kazi kwa mazoea likiendelea huku wananchi wakikabiliwa na matatizo mbalimbali yanayohitaji ufumbuzi kutoka kwa watendaji lakini mengine yamelala kwa zaidi ya miaka 10.

Miongoni mwa mambo aliyokutana nayo Makonda ni gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya afya, maji na elimu zilizoonyesha kuwapo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za serikali.

Kutokana na kuwapo kwa madudu hayo, mkuu huyo wa mkoa ametamka bayana kwamba hatakuwa radhi na watu wa aina hiyo ambao wanakwamisha juhudi za serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo. Ameagiza mamlaka husika kuwachukuliwa watu hao hatua zinazostahili ili kurejesha nidhamu katika utendaji kazi na usimamizi wa mali za umma.

Aidha, juzi katika ziara hiyo, akiwa wilayani Monduli, alisema hatishwi na kauli za watu wakiwamo wanasiasa kupitia mitandao ya kijamii kwamba anafanya baadhi ya mambo kwa kukiuka haki za binadamu, ikiwamo kauli anazozitoa kwamba baadhi ni za udhalilishaji. Makonda aliapa kwamba kelele hizo hazimfanyi kuendelea na jitihada zake za kuchukua hatua dhidi ya wezi, wabadhirifu, wavivu na wazembe na kusisitiza kwamba atawapiga spana (atawabana) watu hao.

Suala la watendaji serikalini kutimiza wajibu wao kwa viwango na weledi pamoja na kutatua kero za wananchi katika maeneo waliyoko, limekuwa likisisitizwa na viongozi wa ngazi za juu serikali wakiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na naibu wake, Dk. Doto Biteko. Kwa mantiki hiyo, Makonda anachokifanya ni marudio ya yale yanayofanywa na wakuu wake.

Kwa ujumla, tangu apewe wadhifa huo zikiwa hazijafikia siku 100, Makonda ameibua madudu ambayo yako kila mahali huku watendaji wakiwa wamelala usingizi wa pono, wakishindwa kushughulikia kero za wananchi ambao wanapaswa kuwatumikia kupitia nafasi zao. Hivyo ndivyo inavyotakiwa na kila kiongozi au ofisa wa serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Madai kwamba kauli za Makonda dhidi ya baadhi ya watumishi wazembe, wavivu, wezi na wabadhirifu zinapaswa kuungwa mkono badala ya kushutumiwa. Watanzania wanapaswa kuwatetea watu wa aina hiyo kwa mwavuli wa haki za binadamu badala yake waungane na viongozi wanaokemea mambo na tabia hizo ambazo zimekuwa kikwazo katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Watu wanaotoa kauli hizi wanapaswa kujiuliza kushindwa kutetea na kusimamia maendeleo ya wananchi ni haki za binadamu? Mtu anapoambiwa ukweli ni kudhamilishwa? Katika maisha, iwe utumishi au kazi, kuna haki na wajibu, hivyo mtu anaposhindwa kutimiza wajibu na kuelezwa ukweli asifichwe na kutetewa kwamba amedhalilishwa na kazi zake za msingi zimevunjwa.

Inawezekana kuna baadhi ya kauli anazotoa Makonda ni za udhalilishaji lakini hakuna budi kujiuliza zimetokana na nini badala ya kumshutumu tu. Ni vyema kila mtu akasimama katika nafasi yake badala ya kuendelea kuwalinda na kuwatetea watu wanaokwamisha jitihada za serikali kuwaletea maendeleo kwa kivuli cha haki za binadamu.



## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# HESLB itimize ushauri huu

**HIVI** karibuni iliibuliwa hoja bungeni, kuhusu utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kwamba serikali iwafuatilie mitaani kubaini idadi ya vijana walioacha kuendelea na masomo ya vyuo vikuu na kurudi nyumbani kutokana na wazazi au walezi kushindwa kuwagharamia.

Mbunge wa Ngara, mkoani Kagera, Ndaisaba Ruhoro andiye mwenye hoja hiyo ambaye anaongeza kuwa serikali ikishawapata iwapeleke Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ili wapatiwe mikopo na kuendelea na masomo ili kutimiza ndoto zao za kujiendeleza kielimu.

Anasema, hali imekuwa mbaya zaidi kama ilivyo katika ngazi za chini, kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi kuacha masomo, na sasa kibao kimegeukia upande wa vyuo vikuu, kwa wanachuo kuacha masomo.

Kwa hoja hiyo, ninaungana na mbunge huyo, kwani pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali kuboresha elimu, bado kumekuwapo na malalamiko kwenye suala la mikopo ya elimu ya juu.

Imekuwa ikielezwa kuwa pamoja na serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, wapo baadhi ya wanafunzi ambao wamekuwa wanakosa licha ya kuwa na vigezo vya kupata ufadhili huo.

Nadhani wakati sasa wa HESLB kuhakikisha wanafunzi wanapata mikopo hiyo bila usumbufu, kwani lengo la bodi hiyo ni kuwezesha kusoma elimu ya vyuo vikuu na vyuo vya kati.

Nipashe ilishawahi kuzungumza na wanafunzi waliolalamika kunyimwa au kupatiwa mkopo 'kiduchu', lakini Mkuu wa Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole, akabainisha kuwa mwaka huu wa masomo, hakuna mwanafunzi aliyepatiwa mkopo kwa asilimia 100 isipokuwa waombaji wenye ulemavu na wale waliopoteza wazazi wote wawili.

Uamuzi wa bodi wa kutoa mkopo wa asilimia 100 kwa wanafunzi wenye ulemavu na waliofiwa wazazi wote ni sawa, lakini inawezekana pia wapo baadhi ya wanafuzni wakawa na wazazi wote lakini hawana uwezo.

> **Nadhani wakati sasa wa HESLB kuhakikisha wanafunzi wanapata mikopo hiyo bila usumbufu, kwani lengo la bodi hiyo ni kuwezesha kusoma elimu ya vyuo vikuu na vyuo vya kati.**

Vilevile inawezekana baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu, wanatoka katika familia zenye uwezo, hivyo, ni vyema kuendelea kufuatilia hilo kwa karibu ili kupunguza idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo.

Hivyo, litakuwa jambo jema iwapo kutakuwa na ufuatiliaji wa karibu suala hilo la mikopo ya elimu ya juu ili kama itawezekana, basi wanafunzi wote wapewe ili waweze kutimiza ndoto zao katika elimu.

Lakini pia, kwa kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda alishasema serikali inakaribisha taarifa za wananchi kwa ajili ya uchunguzi unaoendelea kuhusu mchakato wa kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu, basi wajitokeza kusaidia katika hilo.

Ni wakati akielezea uamuzi wa serikali kuunda timu ya kuchunguza mchakato wa utoaji wa mikopo, kwa ajili ya wanafunzi hao ili kubaini changamoto na kutoa ushauri.

Kimsingi, lengo ni kuondoa changamoto katika utoaji wa mikopo hiyo kama zipo, na inawezekana kukawa na mawazo mazuri zaidi yatakayosadia kuboresha mikopo hiyo.

Lakini pia, hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali imeongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 654 kwa mwaka 2022/23 hadi Sh. bilioni 738.7 mwaka 2023/24.

Katika hilo wakati wa hotuba yake bungeni jijini Dodoma, alisema wanufaika wa mikopo na ruzuku wameongezeka kutoka 177,615 mwaka 2022/23 hadi wanafunzi 220,278 mwaka 2023/24.

Ninaamini hatua inaweza kuwa inalenga kuhakikisha wanafunzi wote wananufaika na mikopo hiyo bila kuwaacha wengine nyuma kwa vigezo ambavyo wakati mwingine vinaweza kuwaumiza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

HABARI KITAIFA

# Muhimbili yaweka rekodi mpya ikipandikiza uloto

**Na Christina Mwakangale**

WAGONJWA watano waliopandikizwa uloto wameruhusiwa kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila siku 14 baada ya upandikizaji.

Kuruhusiwa kwa wagonjwa hao watano (wanawake wawili) wenye umri kati ya miaka 40 hadi 56 kuruhusiwa jana, kunafanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma hiyo kufikia 16 tangu kuanza matibabu ya aina hiyo nchini Novemba 2021.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema huduma hiyo imegharimu Sh. milioni 60 kwa mgonjwa. Kama wangepelekwa nje ya nchi, matibabu yao yangegharimu Sh. milioni 150 hadi 200 kila mmoja.

"Huduma hii bobezi na ya kibingwa inatokana na uwekezaji wa serikali. Upandikizaji uloto ambao kimsingi kwa lugha rahisi ni saratani ya damu ni ghali, matibabu haya yana hatua nyingi. Serikali inachangia asilimia kubwa.

"Kuna ambao wapo wanasubiri kupandikiza ambao ni 150. Baada ya kufanikisha kwa hawa 16, MNH inaongoza kwa wingi wa upandikizaji katika eneo zima la Afrika Mashariki, Kati, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukiiacha Afrika Kusini," alisema Prof. Janabi.

Alisema uchunguzi huanzia MNH-Upanga kisha upandikizaji hufanyika Mloganzila kuliko na vyumba maalum kwa wagonjwa wa aina hiyo; matibabu kuhusisha kuvuna, kuchakata, kupandikiza chembe hai 'mama' (stem cells) ambazo hutolewa kwa wagonjwa walio na saratani ya damu (leukemia, multiple myeloma, lymphoma).

Prof. Janabi alisema matibabu kama hayo pia hutolewa kwa wanaoshindwa kuzalisha chembe hai za damu (aplastic anaemia) pamoja na thalassemia na selimundu.

"Wagonjwa wanaotakiwa kupandikizwa uloto ni wenye changamoto ya saratani ya damu, uloto kushindwa kufanya kazi ya kuzalisha chembechembe za damu na wenye selimundu," alisema.

Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Upandikizaji (Haematologist &Bone Marrow Transplant), MNH-Mloganzila, Dk. Mbonea Yonazi, alisema upandikizaji ulifanyika kwa saa moja na nusu huku wagonjwa hao wakikaa hospitalini kwa siku 14.

Alisema kuwa baada ya upandikizaji, siku ya sita tangu mgonjwa kufanyiwa upandikizaji uloto zinakuwa na changamoto kutokana na mwili kuanza kukabiliana na mapokeo ya mfumo mpya mwilini.

"Wagonjwa wataendelea kuhudhuria kliniki baada ya kuruhusiwa. Kila mwezi watafika hospitalini kwa ajili ya kliniki, ila ni imani yetu kama walivyopandikizwa wale 11 awali hawakupata changamoto, nao watakuwa sawa, wafuate ushauri," alisema bingwa huyo.

Deogratias Mwolo, miongoni mwa watano waliopandikizwa uloto, alisema kwamba awali baada ya kubainika ana saratani ya damu na gharama za matibabu ni kubwa, alipata shida kupokea taarifa hizo.

"Nilipoambiwa mara ya kwanza vipimo vyangu vinaonesha ni saratani ya damu, masikio yangu yaliziba kwa muda. Nikajiuliza ninaambiwa ukweli, ni mimi au? Gharama ya kutibiwa ni kubwa, nilichanganyikiwa," alisema Deogratias.

Alisema anaishukuru serikali kufanikisha huduma hiyo pamoja na timu ya madaktari kutokana na kuwapa huduma nzuri yeye pamoja na wenzake wanne.




Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi (katikati waliokaa), akizungumza na waandishi wa habari, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu wagonjwa watano (waliosimama nyuma), walioruhusiwa kutoka MNH-Mloganzila, baada ya kupandikizwa uloto. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# 'Uchunguzi wa ajali kiwanda cha sukari Mtibwa ukamilike haraka'

**Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Deogratius Ndejembi, ameagiza Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kukamilisha uchunguzi wa ajali iliyotokea kiwanda cha kuzalisha sukari cha Mtibwa ili kuruhusu kiwanda hicho kurejea katika uzalishaji.

Alitoa maagizo hayo juzi baada ya kutembelea eneo la ajali na kupatiwa maelezo juu ya ajali hiyo na uongozi wa kiwanda pamoja na taarifa ya awali ya uchunguzi wa OSHA.

"Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa uongozi wa kiwanda kutokana na athari kubwa za ajali hii iliyogharimu maisha ya wataalamu 13 pamoja na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya kiwanda.

"Niseme tu kwamba huu si wakati wa kumtafuta mchawi bali ni wakati wa kufanya uchunguzi na tafakari ya kina ili kung'amua chanzo cha tatizo lililojitokeza kwa minajili ya kufanya maboresho yatakayozuia janga kama hilo au mengine kujitokeza tena.

"Nizipongeze taasisi chini ya ofisi yangu zinazohusika katika suala hili hususan OSHA kwa kuchukua hatua za haraka katika kushughulikia jambo hili na niwatake kukamilisha taarifa ya uchunguzi wa ajali hii haraka sana ili kuruhusu maboresho ya miundombinu ya kiwanda kufanyika na uzalishaji kuendelea kuepuka athari zaidi kiuchumi kutokana na uzalishaji sukari kutofanyika, hasa tukizingatia kiwanda hiki kinategemewa na wakulima wengi ambao huuza miwa yao hapa," alieleza.

Akitoa taarifa kwa waziri kuhusu ajali hiyo, Meneja Msaidizi wa Kiwanda hicho, Juma Saidy, alisema ajali hiyo ilitokea wakiwa wanafanya makabidhiano ya mtambo wa kufua umeme kwa njia ya mvuke (steam turbine) wenye uwezo wa kuzalisha kilowati 15 za umeme kutoka kilowati sita za awali, lengo likiwa kuongeza uzalishaji sukari.

Kwa mujibu wa Saidy, mtambo huo ulikuwa unalishwa na mtambo mpya wa kufua mvuke Na. 4 (Steam Boiler No.4), wenye uwezo wa kuzalisha mvuke wa tani 125 kwa saa, joto linaloweza kuzalishwa linafikia nyuzi joto 450.

"Saa saba usiku wa kuamkia tarehe 23 Mei mwaka huu, wakati makabidhiano yanayotokana na kubadilisha mfumo wa awali wa kufua umeme yakiendelea, ndipo ajali ilipotokea katika eneo la mtambo wa kuzalisha umeme (power house)," alisema Saidy.


Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema tathmini ya awali iliyofanywa na wataalamu wake ambao walifika katika eneo la tukio tangu Mei 23 inaonesha chanzo cha ajali ni kupasuka kwa kiungio (bellow) ambacho ni sehemu ya mfumo wa uhimilivu wa mitetemo (Gimbal Expansion Joint).

Aliongeza kuwa mpasuko huo ulisababisha kufumuka kiungio hicho kutokana na msukumo mkubwa wa mgandamizo wa mvuke ambao ulisababisha vifo vya papo hapo kwa wafanyakazi 11 na majeruhi wawili ambao walifariki dunia Mei 24 wakiwa wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Benjamini Mkapa, jijini Dodoma.

Kiongozi huyo wa OSHA aliahidi wataalamu wake watakamilisha uchunguzi huo haraka iwezekanavyo na kutoa ushauri wa kina juu ya maboresho yanayohitajika katika kuzuia changamoto iliyotokea kujirudia au changamoto nyingine kutokea.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Vijana wenye ubunifu waitwa NMB

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

BENKI ya NMB imeshiriki maadhimisho ya elimu, ujuzi na ubunifu yanayoendelea kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlaly, ikitoa fursa kwa vijana wenye ubunifu kwenda kufanya majaribio katika mfumo maalum wa benki hiyo.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Baraka Ladislaus, alitangaza fursa hiyo wakati wa ufunguzi wa maadhimisho hayo, mgeni rasmi akiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliyesema benki hiyo inatambua umuhimu wa ubunifu katika maendeleo ya nchi.

Ladislaus alisema benki hiyo pamoja na ufadhili wa maonesho hayo, pia inatoa jukwaa maalum na kukaribisha vijana kufanya ubunifu kwa kuwa benki imekuwa inafadhili maendeleo ya kibunifu na miradi hiyo.

"Kwa niaba ya Benki ya NMB niwaambie kwamba tunatambua umuhimu wa ubunifu na ndio maana tumeungana nanyi katika wiki hii kwa kuwa elimu ndio inachochea ubunifu sisi kama benki pamoja na ufadhili, tunatoa jukwaa maalum kukaribisha vijana kuja kufanya ubunifu kufanya maendeleo ya kibunifu na miradi itakayokuwa bora zaidi basi tutaifadhili," alisema meneja huyo wa Kanda ya Kaskazini yenye mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Alisema benki kwa kufanya hivyo inasaidia kuleta chachu ya kuendelela kuleta maendeleo ya ubunifu Tanzania, hivyo wataendelea kuwaunga mkono kuhakikisha maendeleo ya sekta hiyo yanapiga hatua kubwa.

"Niwakaribishe vijana wenye ubunifu mbalimbali waje kufanya majaribio yao kwenye Benki ya NMB, tuna jukwaa la NMB Sandbox zuri ambalo linatoa nafasi nzuri ya ubunifu, tupo tayari kushirikiana nao ili kuhakikisha ubunifu unaleta chachu ya maendeleo ya kiuchumi nchini, alisema.

Awali akizungumza wakati akifungua maadhimisho hayo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Mkenda, alisema serikali ipo katika mchakato wa kujenga shule 100 za mafunzo ya amali nyanja ya ufundi nchi nzima ili kuwezesha vijana wa Kitanzania kujiajiri au kuajiriwa kupitia ujuzi watakaopata kupitia vyuo hivyo.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema dunia ya sasa ina mabadiliko makubwa hasa kwenye masuala ya sayansi na teknolojia, ujuzi na ubunifu, hivyo ni wakati wa vijana wa Kitanzania kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Mwenyeji wa Maadhimisho hayo, Balozi Dkt. Batilda Buriani, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, alisema mkoa huo umepokea Sh. trilioni 2.06 kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu ambapo shule mpya 27 zimejengwa pamoja na vyuo vya kati ambavyo vipo katika hatua mbalimbali.

NMB
Karibu yako

**TAARIFA KWA WANAHISA WA NMB**
**UBORESHAJI WA TAARIFA ZA KIBENKI NA NAMBA YA MLIPA KODI (TIN)**

Benki ya NMB inapenda kuwataarifu wanahisa wake kuwa wanatakiwa kuboresha taarifa zao ikiwemo akaunti ya benki, taarifa za mawalisiliano ikiwa pamoja na taarifa za ndugu au jamaa wa karibu na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN) ili kuwezesha benki ya NMB kulipa gawio kwa wakati.

**Maboresho haya ni mahususi kwa wanahisa wa NMB:**

i. Ambao hawajawasilisha namba ya mlipa kodi (TIN) kama inavyotakiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
ii. Wanahisa wote wapya wa benki ya NMB ambao taarifa zao hazipo benki.
iii. Ambao wamebadilisha akaunti zao za kupokelea gawio na hawajaitaarifu benki.
iv. Ambao hawajapokea gawio lililopita la hisa za NMB.
v. Ambao wamebadilisha taarifa za mawasiliano (mf. namba ya simu, taarifa za ndugu au jamaa wa karibu).
vi. Ambao akaunti zao zimefungwa au hazijatumika kwa muda mrefu.

Wanahisa wanaombwa kujaza fomu ya mwanahisa inayopatikana tawi lolote la NMB lililopo karibu yao. Fomu hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Benki **www.nmbbank.co.tz.**

Tafadhali ambatanisha nakala ya kitambulisho (Kitambulisho chaTaifa/uraia, Mpiga kura au hati ya kusafiria) na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN).

**Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia**
Namba ya simu: +255 22 232 2913
Barua Pepe: Dividend_Unit@nmbbank.co.tz

**NMB Plc – Makao Makuu**
Ohio/Ali Hassan Mwinyi
Ghorofa ya Kwanza - Kitengo cha Mahusiano ya Wawekezaji
S.L.P 9213, Dar es Salaam, Tanzania

www.nmbbank.co.tz

## Mkurugenzi DIB adai Marekani imezuia bilioni 145/- za FBME

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Isaack Kihwili, amedai kucheleweshwa utekelezaji amri ya mahakama kulipa Sh. bilioni 145 ni uamuzi wa mamlaka za Marekani kuzuia kiasi kikubwa cha fedha za Benki ya FBME Ltd kwa tuhuma za kujihusisha na utakatishaji fedha.

Mahakama Kuu Dar es Salaam imesema haijawahi kukumbana na serikali yoyote ya nje kutokuheshimu hukumu ya mahakama.

Kihwili alidai hayo jana mbele ya Jaji Mfawidhi Salma Maghimbi wa Mahakama Kuu alipofika kujieleza kwanini hajatekeleza hukumu iliyotolewa kwa manufaa ya Kampuni ya Coast Textile Ltd miaka tisa iliyopita.

Alidai wameanza kuwasiliana na mamlaka nchini Marekani ili kuondoa vikwazo dhidi ya fedha zilizochukuliwa.

"Tunachokifanya kwa sasa ni kuwasiliana na mamlaka nchini Marekani ili kuondoa vikwazo vya fedha za Benki ya FBME, ambazo zinazuiliwa kwa tuhuma za kujihusisha na utakatishaji fedha," alidai.

Pia alidai wameanza kufanya malipo ya awali kwa wenye amana na kamati ya ukaguzi wa wadai imeundwa na imekutana mara mbili kupendekeza uidhinishwaji malipo hayo.

"Aprili 19, 2024, kamati ilipendekeza malipo kwa wenye amana 500. Mei 22, 2024, kamati ilikutana na kuidhinisha malipo kwa wenye amana wengine 352 ambapo asilimia 30 ya madai yao yamekamilika," alidai.

Pia alidai kuwa wanasubiri wadai wengine wawasilishe madai yao. Utaratibu uliopo unaelekeza wenye amana wote walipwe kwanza kwa asilimia 100 kabla ya wadai wengine, akiwamo mshinda tuzo, ambaye ni Kampuni ya Coast Textile Ltd.

Alidai kuwa wameingia makubaliano na mfilisi wa Benki ya FBME Tawi la Cyprus kugawana mapato baada ya kukusanya fedha kutoka vyanzo mbalimbali ambazo nyingi zinazuiwa kupitia Cyprus. Tanzania itapokea asilimia 12.

Jaji Maghimbi alishauri Mkurugenzi wa DIB kutoa kwa mamlaka husika nchini Marekani orodha ya wadai wa Benki ya FBME yenye hukumu za mahakama, ambao kwa sasa ni wanne, ikiwa ni pamoja na Coast Textiles Limited.

Wakili Joseph Rutabingwa wa Coast Textile Limited aliunga mkono ushauri uliotolewa na mahakama kwa Mkurugenzi wa DIB.

Jaji alimpa Mkurugenzi wa DIB hadi Julai 5, 2024 kutoa taarifa mahakamani kuhusu matokeo ya ulipaji kwa wadai wenye hukumu mkononi kufuatia ushauri uliotolewa na mahakama.

Mei 20, 2022, Jaji Amir Mruma aliamuru Mkurugenzi wa DIB, ambaye aliteuliwa na BoT kama mfilisi wa FBME, kulipa kiasi hicho baada ya kukubali maombi ya utekelezaji hukumu yaliyowasilishwa na Coast Textiles Limited.

## HABARI KASKAZINI



# Wachimbaji madini tanzanite hawana maji wala zahanati

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala, amesema wachimbaji wa madini ya tanzanite Mererani Manyara wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji pamoja na zahanati, hali inayowasababishia kuzorota shughuli za uchimbaji.

Alibaini hali hiyo juzi alipofanya ziara ya kutembelea migodi ya kitalu C inayomilikiwa na Kampuni ya Franone Mining and Gems Ltd, Kitalu A kinachomilikiwa na Kilimanjaro Mining, Gems & Rock na mgodi wa Saniniu Laizer.

Lulandala alisema huduma hizo zinahitajika kwa haraka kwa kuwa zina umuhimu kwa wachimbaji hao.

Alisema huduma ya majisafi na salama pamoja na zahanati, ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya tanzanite ni jambo linalotakiwa kutekelezwa kwa haraka kwa kuwa kuna msongamano wa watu wengi.

Aidha, alisema ni vigumu kusukuma na kusimamia usichokifahamu au kukijua, hivyo kufika kwake kutembelea migodi hiyo, amefahamu baadhi ya changamoto muhimu zinazotakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka ili jamii ipate huduma.

"Nilichofanya ni kupita sehemu mbalimbali ndani ya ukuta, kuanzia kwa Ofisa Madini Mkazi Mirerani, Chacha Marwa Nchagwa, maeneo ya kimkakati na ya kiungalizi yanayohusiana na eneo letu la migodi," alisema Lulandala.

Hata hivyo alisema akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Simanjiro wamepita maeneo mengine ya kawaida ya kijamii kwa kuwa kuna shughuli nyingi zinaendelea kufanyika maeneo mbalimbali ndani ya Mirerani.

Alisema: "Nilitaka kufahamu huduma za kijamii ndani ya migodi, kuona wingi wa watu wanavyoishi na wanachofanya, tukaona ni vizuri tupite tujifunze, sijapita kuja kusikiliza kero, ila nitakuwa na utaratibu wa kusikiliza kero na kupokea ushauri".

Pia alisema ni vema wananchi wakaiamini serikali inavyofanya kazi kwa lengo la kuharakisha maendeleo na kutambua mchango unaofanywa na wachimbaji madini ya tanzanite.

Alisema: "Mimi ni mkuu wenu wa Wilaya ya Simanjiro, tuko hapa kumwakilisha Rais Samia kwa niaba yake na nyie wote na shughuli zenu mbalimbali ni wapigakura wake, kwa hiyo sisi tunawajibika kufika kwenu kuwasikiliza."

# TAKUKURU 'yamnyofoa' mkurugenzi Arusha dhidi ya tuhuma za rushwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Arusha, imemsafisha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Juma Hamsini, kwa kumwondoa kwenye tuhuma zilizokuwa zinamkabili.

Hatua hiyo imekuja baada ya uchunguzi wa awali kuonesha hahusiki na tuhuma hizo ikiwamo kughushi nyaraka, kuchepusha makusanyo ya serikali na ubadhirifu wa fedha za umma.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa TAKUKURU mkoani Arusha, Zawadi Ngailo, alisema uchunguzi wa awali uliofanywa na umebaini kuwa mkurugenzi huyo na wenzake hawakuhusika moja kwa moja na tuhuma zilizoibuliwa na mfanyabiashara Wilbard Chambulo.

Chambulo aliibua tuhuma dhidi ya mkurugenzi huyo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda ambaye aliagiza taasisi hiyo kufanyia kazi tuhuma hizo.

Tuhuma zingine zilizoibuliwa ni uwepo wa kampuni hewa, malipo hewa na namba bandia za mlipakodi zilizotumika kuchepusha kodi na mapato ya halmashauri ya jiji la hilo.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini watumishi wawili wa halmashauri hiyo, wamehusika kughushi nyaraka ikiwamo kutengeneza namba bandia ya mlipakodi na kutumia kampuni hewa kulipia mapato.

Ngailo alisema kutokana na maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, Aprili 13, tayari taasisi hiyo ilikuwa imeshaanza uchunguzi wao wa awali toka siku ya kwanza walipopata malalamiko hayo.

"Maelekezo yalitolewa kwenye kikao kati ya Mkuu wa Mkoa na wafanyabiashara wa sekta ya utalii mkoani Arusha, ofisi yangu ilikuwa tumeshaanza uchunguzi na uchunguzi huo ulikuwa unahusisha idara ya mapato (ushuru wa huduma) katika Halmashauri ya Jiji la Arusha," alisema.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa bado wanaendelea na uchunguzi na pindi watakapokamilisha wahusika (hakuwataja majina yao) watafikishwa mahakamani.

TAKUKURU ilianza kufanya uchunguzi wa agizo lililotolewa na Makonda kufuatia tuhuma zilizowasilishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Wilbard Chambulo, akilalamikia kulipa kodi ya huduma Sh.milioni 24, lakini alipewa risiti ya Sh.milioni 3.6 kitu ambacho kilimshangaza.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwenye account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia


**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian





# Mradi majitaka kunufaisha wakazi 7,000

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKAZI 7,300 pamoja na kaya 1600 mkoani Mwanza wanatarajia kunufaika na utekelezaji wa mradi wa miundombinu ya majitaka utakaosaidia kukabiliana na hali ya uchafuzi wa mazingira na Ziwa Victoria.

Mradi huo unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) chini ya ufadhili wa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania, Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya KfW na Umoja wa Ulaya (EU), kupitia programu ya pamoja ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Bonde la Ziwa Victoria (LVB-IWRM).

Hayo yameelezwa juzi jijini hapa katika kikao baina ya MWAUWASA, LVBC na ujumbe kutoka Benki ya Maendeleo ya Ujerumani ukiongozwa na Mkurugenzi wa KfW Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika, Christoph Tiskens.

Akizungumza katika kikao hicho, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Neli Msuya, alisema dhamira ya mradi huo ni kuhakikisha mazingira katika Ziwa Victoria yanahifadhiwa kwa kuwa na mfumo rafiki wa uondoshaji majitaka hususani katika maeneo ya miinuko.

"Mradi utawezesha ukarabati na upanuzi wa mtandao wa majitaka wa kilomita 14.4 sambamba na ukarabati wa miundombinu ya majitaka, uboreshaji vituo vya kusukuma majitaka na ununuzi wa vifaa vya usimamizi wa mfumo wa majitaka yakiwemo magari ya kuondoa majitaka majumbani hasa katika maeneo ya Pasiansi, Kitangiri, Nyamanoro, Kirumba na Igogo," alisema Msuya.

Mkurugenzi wa KfW, Christoph Tiskens alipongeza hatua za miradi iliyotekezwa pamoja na mapokeo ya watumiaji na kuthibitisha kuwa benki hiyo itaendelea kufanya kazi na MWAUWASA katika utekelezaji wa miradi hiyo muhimu kuinusuru jamii na uchafuzi wa mazingira pamoja na Ziwa Victoria.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**

**INAYOKETI DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOBI YA MADAI NA. 56/01 YA 2019**

**INTERNATIONAL SCHOOL OF TANGANYIKA.......................... MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH ERNEST MANGUKU NA WENZAKE 31 ................ WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**

**1.MIKIDADI MUSSA,**
**2.BONIPHACE MWAKYALABA,**
**3.MAJUTO JUMA NA**
**4.HALFAN LAMULIZA**

**POPOTE MLIPO**

Mnajulishwa kwamba shauri la Maombi ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es salaam tarehe 11/06/2024 saa tatu kamili asubuhi (3:00).

Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyie wenyewe au mwakilishi wenu anayetambulika kisheria basi Maombi ya muombaji yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16/05/2024.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

**A. S. CHUGULU**
**Kny: MSAJILI**
**MAHAKAMA YA RUFANI**


# Wananchi walalamika kuletewa bili feki za maji

**Na Alex Sayi,** MASWA

BAADHI ya wanachi wilayani Maswa, mkoani Simiyu wameulalamikia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani hapa kwa kuwabambikizia bili za maji.

Malalamiko hayo yameibuka juzi katika mkutano wa wananchi na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika Kata ya Kadoto.

Joyce Hilya alisema licha ya nia ya serikali kuhakikisha inamtua mwanamke ndoo kichwani lakini kumekuwepo na tatizo katika utekelezaji wa zoezi hilo ikiwa ni pamoja na kupandishwa kwa gharama za huduma kutoka Sh.30 na Sh.50 hadi Sh.70 kwa ndoo moja.

Vilevile alisema mita zilizofungwa zimekuwa zikitumika kuwabambikizia bili watumia wa maji hayo, kwani kuna muda wanalazimika kufunga mabomba kutokana na ongezeko la bei kwa kipindi cha mwezi mmoja au miwili lakini bado wanaletewa bili ambayo hawajatumia.

Akijibu malalamiko hayo, Meneja wa RUWASA wilayani hapa Lucas Madaha aliahidi kufuatilia suala la ongezeko la bei kwa watoa huduma ya maji ngazi ya jamii katika kata hiyo.

Alisema tayari walishatoa bei elekezi ya kuchota maji kwa miradi inayotumia mfumo wa umeme kuwa ni Sh.40 kwa ndoo.

Alisema kwasasa wamekuja na mfumo wa kulipa kwa mfumo wa elektroniki ambao ni shirikishi ambao unamhusisha mtumiaji wa maji katika usomaji wa mita na kujihakikishia huduma anayoilipia.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Nawanda alimtaka Meneja RUWASA Wilaya kuhakikisha CBWSO zinafuata bei elekezi ya ndoo ambayo ni Sh.40 kwa miradi ya maji inayotumia mfumo wa umeme, ili kundoa malalamiko kwa watumiaji wa huduma hiyo.

# Wamiliki viwanda walalamikiwa kutiririsha maji ya kemikali

**Na Shaban Njiia,** KAHAMA

MADIWANI katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamewalalamikia wamiliki wa viwanda vya kuchenjua madini ya dhahabu kutiririsha maji ovyo yenye kemikali ya zebaki, ambayo yanasababisha mifugo kufa pindi wanapokunywa.

Walibainisha hayo juzi kwa nyakati tofauti wakati wakijadili na kutoa taarifa za maendeleo ya kila kata katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri hiyo.

Diwani wa Kata ya Lunguya, Benedicto Manwali alisema, idadi kubwa ya viwanda hivyo havina uzio na mifumo ya majitaka, hali inayosababisha utiririshaji wa maji hayo kwenye maeneo ya marisho.

Manwali alisema maafa ya mifugo kufa yamekuwa yakijitokeza katika viwanda vilivyopo katika Kata za Lunguya na Segese na kuiomba serikali kuingilia kati na kudhibiti majanga hayo na kuchukua hatua dhidi ya watiririshaji hao.

Diwani wa Viti Maalumu, Hamisa Kalinga alisema hali hiyo inahatarisha pia afya za wananchi husani katika mfumo wa fahamu, figo, uwezo wa kuona, mikono kutetemeka, mimba kutoka.

Alitaja athari nyingine ni watoto kuzaliwa na utindio wa ubongo na kuchanganyikiwa hivyo kunaulazima wa wamiliki wa viwanda hivyo kudhibitiwa.

Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira Halmashauri hiyo, Salehe Lyulu alikiri kuwepo kwa hali hiyo na kueleza kuwa tayari ametoa muda wa mmoja kwa wamiliki kuhakikisha wanajenga uzio na mifumo ya maji taka ili kukabiliana na hali hiyo.

# Gari lenye shehena ya mirungi lakamatwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limekamata gari iliyobeba dawa za kulevya aina ya mirungi viroba 25, huku dereva akitokomea kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Janeth Magomi alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa jeshi hilo linaendelea kumsaka dereva wa gari hilo pamoja na mmiliki.

Alisema mirungi hiyo ilikamatwa katika gari moja ambalo liligonga ng'ombe maeneo ya Bugweto Manispaa ya Shinyanga, na askari walipofika eneo la tukio na kufanya ukaguzi ndipo wakakuta viroba 25 vya mirungi, huku dereva akikimbia.

Aidha, alisema kuwa kupitia msako uliofanyika kuanzia Aprili 17 hadi Mei 27 mwaka huu walikamata dawa za binadamu zilizoisha muda wake zilizokuwa zikiuzwa katika mojawapo ya duka la dawa katika Manispaa ya Shinyanga.

"Tulikamata pakiti 86 za dawa hizo ambapo mtuhumiwa anaendelea kushikiliwa kwa hatua zaidi za kisheria,"alisema Magomi.


Alitaja bidhaa nyingine zilizokamatwa kuwa ni pamoja na televisheni moja, mzani mmoja, redio moja, pikipiki 16 pamoja na pombe haramu aina ya gongo lita 20.

Kuhusu usalama barabarani, Kamanda Magomi alisema walikamata makosa 6,320 upande wa pikipiki, huku magari yakiwa ni 4,847, bajaji na pikipiki 1,473 ambapo wahusika waliwajibishwa na kulipa faini ya papo kwa papo.



Ukurasa 13

**RAIS SAMIA ALIVYO TURUFU USHINDI WA UPINZANI 2025**



Ukurasa 14

**Uchaguzi A/Kusini 2024: ANC hoi, hatihati kuanguka**

siasa

JUMATANO MEI 29, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

NI JAMBO JIPYA TLP

# Uchaguzi Mwenyekiti Taifa waiva kufanyika mwezi ujao

**Na Sabato Kasika**

HUENDA mwezi ujao ukawa mwisho wa vuta ni kunivute iliyokitafuna Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), baada ya kifo cha Mwenyekiti wa Taifa, Augustine Mrema, mwaka juzi.

Ni kwa muda mrefu kumekuwa na mvutano na mzozano kati ya Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo na Mwenyekiti wa Vijana wa TLP Taifa, Aivan Manganza, huku kila mmoja akiwa na kundi lake, kuzungumzia hatima ya uchaguzi wa kiongozi huyo mkuu.

Mvutano huo, ulianza mwanzoni mwa mwaka jana, baada ya kuahirishwa kwa uchaguzi wa mwenyekiti wa taifa wa chama hicho na kusababisha wajumbe na baadhi ya viongozi kugawanyika.

Baada ya mvutano wa muda mrefu, hatimaye viongozi wa chama hicho, wamekutana katika kikao cha pamoja na kukubaliana kufanya mkutano mkuu wa uchaguzi wa mwenyekiti wa taifa mwezi ujao-Juni 29.

Wanalenga baada ya mchakato huo kujipanga kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaofanyika mwaka huu na mkuu wa mwakani 2025.

Uamuzi huo ulifikiwa hivi karibuni baada ya viongozi hao kuamua kumaliza vuta nikuvute hiyo ili kukijenga chama upya kijiandae, kwa ajili ya majukumu hayo makubwa ya kitaifa ili kujiimarisha kwenye michakato ya kisiasa na kiuongozi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam Maganza Mwenyekiti wa Vijana Taifa, anasema, yeye na viongozi wenzake wameamua katika kikao maalum cha kujadili hatima ya uchaguzi wa mwenyekiti wa na kufikia uamuzi huo.

"Wote tumekubaliana kwamba uchaguzi ufanyike Juni 29 mwaka huu, ili tujiandae na uchaguzi wa serikali za mitaa na kisha mkuu utakaofanyika mwakani," anasema Maganza.

Mwenyekiti huyo wa vijana anaongeza kuwa kinachotakiwa ni uchaguzi wa kumpata mwenyekiti wa taifa na sio kuendeleza malumbano na mvutano usio na tija unaweza kuendelea kuiumiza TLP.

"Uzuri ni kwamba, wenzetu ambao awali walikuwa hawataki kuitisha uchaguzi, hatimaye wamekubali baada ya kukutana na kujadiliana kwa kina. Lengo likiwa ni ustawi wa TLP," anasema Maganza.

Anaongeza kuwa inauma kuona vyama vingine vikijinadi mikoani, huku TLP kikiendelea na migogoro ambayo si ya lazima na kwamba uamuzi wa kufanya uchaguzi utarejesha uhai wa chama hicho.

"Lakini kwa kuwa tumekubaliana kufanya uchaguzi, naamini tunakwenda kujipanga upya mara tu baada ya kupata mwenyekiti mpya atakayeongoza chama chetu," anasema kiongozi huyo.

Mwenyekiti huyo wa vijana anawataja waliojitokeza kuwania nafasi hiyo kuwa ni mwenyewe Maganza, Richard Lyimo, Stanley Ndamugoba, Kinanzaro Mwanga pamoja na Abuu Changaa.

Katibu wa TLP Taifa, Richard Lyimo, anathibitisha kuwa Juni 29 ni siku ya kufanya uchaguzi huo na kufafanua kwa kifupi kuwa Kaimu Mwenyekiti wa Chama Taifa, Hamad Mkadamu, ndiye aliyewatangazia uamuzi huo.



Aivan Maganza, Mwenyekiti wa Vijana TLP Taifa. **PICHA:MTANDAO**

**KUHUSU DANADANA**

Baada ya kifo cha aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa, Augustino Mrema, Agosti 21, 2022, mwezi uliofuata sekreterieti ya TLP ilimchagua Mkadamu kukaimu nafasi hiyo ili baadaye chama kifanye uchaguzi.

Mara ya kwanza, walijipanga kufanya uchaguzi Januari 8, mwaka jana, lakini ukaahirishwa hadi Machi 6, mwaka huo lakini pia haukufanyika ukapangwa kufanyika Mei mosi 2023, hata hivyo, uchaguzi huo pia ulikwama ukipelekwa hadi Desemba 28 mwaka jana, hata hivyo bila mafanikio, baadaye ukasogezwa hadi Januari 28 mwaka huu, hata hivyo ukapigwa kalenda tena.

Danadana hizo ziliwafanya wajumbe wa Kamati ya Halmashauri Kuu kuja juu kutoa siku saba kwa uongozi kuitisha uchaguzi, vinginevyo wajumbe hao wangelazimika kutisha uchaguzi ambao ungefanyika Februari mwaka huu.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Damary Richard, alitoa siku hizo jijini Dar es Salaam Januari mwaka huu akiwa na baadhi ya wajumbe wakiwataka viongozi wa chama kuhakikisha wanaitisha uchaguzi na Mwenyekiti wa Taifa anachaguliwa.

Damary anaeleza kuwa kutofanyika kwa uchaguzi kunasababisha chama kupoteza hadhi mbele ya Watanzania na kukosa ushawishi kwa kuwa hakijitangazi na kukifanya kisujulikane.

Lawama zake alikuwa akizipeleka kwa kaimu mwenyekiti wa chama hicho, Hamad Mkadamu na Katibu Mkuu Richard Lyimo, kwamba wanaua chama kwa kupinga chenga kuitisha uchaguzi.

"Sasa kwa kuwa tarehe ya uchaguzi imeshatangazwa, ninaamini chama chetu kinakuja kuzaliwa upya na kitakuwa na nguvu, matumaini, ari, ujasiri wa kukiwezesha kujitangaza kwa umma wa Watanzania na kufikia malengo tuliyojiwekea kisiasa," anasema Damary.

**WAJUMBE KUJIGHARAMIA**

Mwenyekiti wa Vijana Taifa Maganza, anazungumzia kuhusu katiba akisema ibara ya 21.3 (a), inaeleza kuwa wanachama na viongozi wote wanajitolea kufanya uchaguzi, hakuna malipo maalum katika vikao na kwamba wanajitolea na hakuna wa kuwalipa wala wa kumdai.

Kutokana na maelezo hayo, akasema katibu na kaimu mwenyekiti wasikwepe kuitisha mkutano wa uchaguzi kwa kigezo cha gharama, kwa kuwa wajumbe wanajigharamia wenyewe na kwamba ibara ya 18.5 (k), inaeleza kuwa kazi ya halmashauri kuu ni kuandaa mkutano mkuu.

Aidha, anarejea katiba ya chama hicho akisema baadhi ya vifungu ikiwamo ibara ya 24, inaelezea kuwa nafasi ikiwa wazi ijazwe mara moja, na kwamba tangu walipopata kaimu mwenyekiti, hadi sasa inapigwa chenga hivyo kukaa kimya ni kukiuka katiba.

# Wadau: Yakifanyika haya R4 za Rais Samia zitajibu



Mwenyekiti wa CUF Taifa, Profesa Ibrahim Lipumba (aliyesimama), akichangia mawazo katika mkutano wa demokrasia jumuishi na shirikishi mjini Zanzibar hivi karibuni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ILI kuyafikia malengo ya falsafa ya 'R nne' za Rais Samia Suluhu Hassan, wadau wanasema unahitajika ufuatiliaji zaidi wa kutekeleza yaliyomo kwenye falsafa hiyo.

Wanataka ufuatiliaji ulenge kuona kuwa taifa linapokaribia uchaguzi mkuu wa 2025 linapata katiba mpya inayoitamani.

Falsa ya R4 ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza; Reconciliation 'Maridhiano', Resilience 'Ustahimilivu', Reform 'Mabadiliko' na Rebuiding 'Kujenga upya'.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, akizungumzia kufanikisha falsafa ya R4, anasema inalenga kukuza na kuimarisha demokrasia hivyo wananchi wanataka malengo yaliyomo ndani yake yatimizwe.

Wakizungumza hivi karibuni kwenye mkutano uliojadili dhana ya demokrasia jumuishi na shirikishi, wanaeleza umuhimu wa kupata katiba yenye maoni ya wananchi.

Kadhalika bila kusahau kufikia lengo la kuwa na taifa lenye mshikamano, utulivu na amani.

Askofu Bagonza akizungumzia kujenga taifa na kuimarisha umoja, anakumbusha kuwa Rais Samia amelitendea haki kwa kuona umuhimu wa kuandaa falsafa ya R4 lakini inaelekea kukwamishwa na baadhi ya viongozi.

Falsafa hiyo ambayo ni msingi wa ujenzi wa demokrasia ikilenga kuleta maelewano na uvumilivu wa kisiasa, kwa mujibu wa Bagonza, haitawezi kufikia ujenzi wa demokrasia bila ya kuvumiliana katika mambo mbalimbali ambayo hutofautiana katika safari ya kuelekea katika uchaguzi mkuu.

Katika jukwaa hilo, wanasiasa wanasema falsafa ya " R 4" ni muhimu ikatekelezwa kwa vitendo kwa lengo la kuona mkwamo wa kisiasa unaondoka hatua ambayo itaimarisha demokrasia na utawala bora, ushiriki mzuri wa mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

> "Ukabila haujawa tatizo letu la msingi, ubaguzi wa rangi haujawa asili katika nchi hii. Taifa lina makabila mengi na nchi mbili, matokeo yake kuna mitazamo mbalimbali ya makundi ambayo yanatufanya kukosa ujasiri wa kupigania kesho yetu," anaongeza.

Mwenyekiti wa kituo cha taasisi ya demokrasia TCD, Professa Ibrahim Lipumba, anampongeza Rais Samia kwa kazi kubwa ya kuimarisha demokrasia, maelewano na utawala bora kupitia R4.

Professa Lipumba, Mwenyekiti wa Chama cha CUF Taifa anasema Rais amejiwekea malengo mahsusi kuhakikisha ujenzi wa demokrasia unaimarika huku akiwa tayari kushirikiana na viongozi wa vyama vya siasa katika mazungumzo yenye maelewano.

Anazungumzia kuundwa kikosi kazi kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mustakabali wa siasa pamoja na kuondoa baadhi ya vikwazo vya kisiasa vilivyokuwapo awali hatima ikawa kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya kisiasa.

"Hayo ni matokeo ya falsafa ya 4R inayosisitiza na kuhimiza maridhiano, majadiliano na mabadiliko makubwa ya demokrasia ambayo ni matokeo ya kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi."

"Falsafa ya R4 lengo lake ni kuwepo kwa demokrasia shirikishi na jumuishi ambayo itafungua milango zaidi na kutoa nafasi ya kuwepo kwa uchaguzi huru na haki," anaongeza.

Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar, Dk.Mohamed Said Dimwa, anasema chama kimeonesha nia ya kufanya mageuzi makubwa ya kisiasa ambayo yatafunguwa milango ya demokrasia na utawala bora.

Kwa mfano, tangu aliposhika madaraka Rais Samia pamoja na Dk. Hussein Ali Mwinyi wameonesha azma ya kufanya kazi na vyama vya siasa kujenga demokrasia na mafanikio yameonekana katika kipindi kifupi.

Dk. Dimwa anavitaka vyama vya siasa kujenga tabia ya kuaminiana na kuondoa hofu miongoni mwao mambo ambayo yanaweza kurudisha nyuma ujenzi wa demokrasia na utekelezaji wa maridhiano ya kisiasa yaliopo.

Anasema serikali ya mapinduzi ya Zanzibar inaundwa na maridhiano ya kisiasa yanayovihusisha CCM pamoja na ACT-Wazalendo na kuhoji anashangazwa na viongozi wanaoitishia kujiondoa katika serikali inayotokana na maridhiano ya kisiasa.

"Maelewano ya pamoja ni muhimu sana ambayo ndiyo tunaweza kufanya mambo mbalimbali muhimu ikiwamo kubadilisha katiba...tuache hofu inaweza kutumaliza kisiasa," anasema.

Mwanasheria mbobezi na mwanaharakati wa haki za binadamu, Dk. Helen Kijo-Bisimba, mbali na kutambua umuhimu wa Tanzania kupata katiba mpya, anaamini hatua za kufikia kileleni lazima ziwe shirikishi na zinazotokana na mipango ya wananchi na sio kuongozwa na watawala.

"Suala hili liwe la watu wenyewe na ni mchakato, sio la kuletewa lakini hapa kwetu mara nyingi tunaona mambo ya katiba yanaletwa na watawala. Tukumbuke wenzetu Kenya na Afrika Kusini katiba ilihusisha wananchi wenyewe," anasema Dk. Hellen Mkurugenzi Mwasisi wa Kituo cha Haki za Binadamu cha Tanzania (LHRC).

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe anasema kutokana na uzoefu wa Kenya na Afrika Kusini katika kupata katiba mpya ilitokana na jamii walikuwa wamoja katika kudai kesho yao.

"Ukabila haujawa tatizo letu la msingi, ubaguzi wa rangi haujawa asili katika nchi hii. Taifa lina makabila mengi na nchi mbili, matokeo yake kuna mitazamo mbalimbali ya makundi ambayo yanatufanya kukosa ujasiri wa kupigania kesho yetu," anaongeza.

Aidha, anasema jambo la kujivunia ni kwamba taifa linazungumza lugha moja katika kuhitaji katiba mpya, hivyo ni vyema kwa pamoja kuwa na msukumo wa kudai katiba mpya ambayo itatoa tiba kwa mambo yanayokwaza.

"Siku moja tufanye maandamano kwa Watanzania wote tunaohitaji katiba bora kwa ajili ya taifa bila ya kujali chama wala dini kuungana katika kudai na kupaza sauti zetu," alisema Mbowe.

Alisema ni vyema kuunganisha nguvu ya pamoja katika kudai katiba na Rais Samia anania njema katika kufanya mabadiliko ya nchi.



Maandamano ya CHADEMA yakisimamiwa na polisi mapema mwaka huu. Lengo ni kuimarisha ulinzi na amani katika kutekeleza jukumu la vyama vya upinzani kufanya shughuli za kisiasa kama Rais Samia Suluhu Hassan, anavyosisitiza. **PICHA: NIPASHE ONLINE**

# Rais Samia alivyo turufu ushindi wa upinzani 2025

**Na Deogratias Mutungi**

HUWEZI kuongelea uwepo wa demokrasia kwa nyakati hizi hapa nchini na hata nje ya mipaka bila kutaja jina la Rais Samia Suluhu Hassan. Inawezekana yapo mengine katika uongozi wake ambayo utayakosoa, lakini kwa hili anastahili maua yake.

Amethubutu na kutenda ikilinganisha na awamu zilizopita, amefungua mifumo ya demokrasia iliyokuwa imedorora kipindi cha awamu ya tano, na sasa mienendo ya siasa imebadilika zaidi.

Anang'ara kidemokrasia sababu kuu ikiwa ni kwa mujibu wa mwenendo wa siasa zilivyo nchini kwa kipindi hiki wala si kwa nadharia za "uchawa" au wasakatonge. Uchawa au wasakatonge, pengine bendera inayofuata upepo ni wale wenye maslahi binafsi na wanafiki kisiasa.

Rais Samia anathibitisha kuwa siasa za upinzani si dhambi, wala kuwa mpinzani si uhaini kisiasa, anadhihirisha kuwa ni uhuni kisiasa kuwabagua wapinzani na kuwajengea nongwa na fitina za fursa sawa.

Amejenga demokrasia na maridhiano akisisitiza kuwa upinzani ni moyo wa maendeleo ya nchi, kwani hukosoa, hushauri na kutoa mwelekeo wa dira iwe kisiasa, kiuchumi na kijamii, hivyo kusulubu upinzani ni ukosefu wa ukomavu katika siasa za mfumo wa vyama vingi.

Wapo wanazuoni, mfano Cicero aliyeandika kitabu akionya "kuuminya upinzani ni msingi na mtaji wa nguvu kisiasa kwa wapinzani, aidha ni kutokujiamini kwa mtawala."

Aidha anasema: "Ni ulimbukeni kupiga hoja ya mpinzani rungu na kwamba hoja zao hujibiwa kwa hoja, wakati takwimu hujibiwa kitakwimu. Kujibu hoja za upinzani kwa rungu na mtutu wa bunduki ni kiburi cha utawala na kutokujiamini kisiasa, mstaafu Jakaya Kikwete, aliwahi kusema hoja haipigwi rungu bali hujibiwa kwa hoja."

Wakati wa kuelekea kwenye chaguzi za serikali za mitaa na mkuu mwakani 2025, kisiasa unaweza kusema turufu ya ushindi kwa vyama vya upinzani imebebwa na Rais, pengine swali la kimantiki linaweza kuwa ni namna gani amebeba ushindi kwa upinzani?

Mosi, tangu achukue uongozi demokrasia imechanua na kustawi ndani na mifumo yake, upepo wa kisiasa umebadilika hila na misuguano baina ya serikali na vyama vya upinzani haipo tena.

Wapinzani wanatabasamu, upinzani si kivuli cha dhambi tena bali mbadala wa serikali katika kusahihishana kwa maslahi ya nchi.

Pili, maamuzi ya Rais Samia kukaa meza moja na upinzani na kufanya maridhiano ya muafaka dhidi ya mustakabali wa siasa ni ishara ya turufu ya ushindi kwa vyama vya upinzani na uamuzi huu wa ni tiketi ya ushindi wa kishindo kwa upinzani kuelekea uchaguzi unaokuja.

Hivyo, vyama vya upinzani ni vyema vikatambua hilo kuwa turufu ya ushindi wao anayo Rais, na endapo atabadili mwelekeo wa siasa kama ilivyokuwa kwa awamu ya tano basi upinzani unaweza kukumbana na rungu zito sawa na kilichotokea kwenye uchaguzi wa mwaka 2020.

Ndiyo wakati walipolia na kusaga meno, ni kipindi ambacho wafuasi wa upinzani walikumbana na nguvu ya asili sawa na kimbuga hidaya.

Sharti ukweli usemwe, awamu ya tano, upinzani ulipotea na kusambaa kama kondoo wasio na mchungaji, hasa baada ya serikali ya John Magufuli kuweka zuio la kufanya mikutano ya hadhara kisiasa, katazo ambalo lilikuwa batili kikatiba.

> "Ni vema kuwa na mawazo mchanganyiko katika shughuli za kisiasa kuliko hoja za upande mmoja. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antoni Guterres anaamini "ufanisi katika uwepo wa kupingana kwa kutoa mawazo na fikira tofauti.""

Matokeo yake ni upinzani na wenye vinasaba vya upinzani kuishi kama shetani au vibwengo kwa kipindi cha miaka sita ndani ya taifa lao, vyama vya hivyo wanajua hilo na historia ya kusulubiwa iliandikwa dhidi yao.

Ni vigumu sasa kulinganisha demokrasia ya kipindi cha mwaka 2016-2020 na nyakati hizi za awamu ya sita. Inakumbukwa hata wapinzani hawakushirikishwa uchaguzi wa serikali za mitaa 2019.

Demokrasia wakati ule ilikwenda likizo ya lazima, na upinzani kupokea kipigo ndizo nyakati Watanzania waliwatofautisha wanasiasa imara na uchwara, upinzani uling'olewa jino bila ganzi na kusulubiwa kwa kivuli cha kuleta maendeleo. Japo kinadharia hamna utafiti unaoonyesha maendeleo huletwa na uvunjaji wa haki za wengine kisiasa au kuminya demokrasia kwa namna yoyote ile.

Japokuwa Afrika ina aina ya demokrasia yake na mara nyingi inavurugwa na watawala bila soni, lakini demokarsia ni nuru ya haki na njia ya utawala bora, uwepo wa mifumo imara ya huimarisha ufanisi wa siasa za vyama vingi.

Kwa pamoja hujenga amani ya kitaifa baina ya serikali na watawaliwa. Kadhalika ombwe la demokrasia huzaa dhuluma ambayo hutengeneza chuki na visasi miongoni mwa jamii na hatimaye kuzaa uasi.

Awamu ya sita imetoa wigo mpana kwa demokrasia kushika hatamu, upinzani unatunisha misuli kadiri uwezavyo, unafanya siasa zao katika mazingira yenye uhuru na usalama zaidi.

Aidha, kauli chanya na hasi zinatolewa na upinzani dhidi ya serikali bila nongwa na bugudha ya namna yoyote ile.

Ni nyakati hizi za Rais Samia ambazo misemo ya zuio la mikutano ya upinzani kwa sababu za "kiintelijensia" imetoweka, kipigo na suluba kwa upinzani hamna tena, kamata kamata imeshasahaulika. Kipindi hiki, mirindimo inayosikika ni hoja za upinzani dhidi ya hoja za chama tawala.

Turufu ya Rais Samia kwa upinzani inawapa ushindi wa asilimia 46 kuingiza wabunge wa kutosha bungeni na wenyeviti wa serikali za mitaa, hivyo mwaka 2026, mizania ya kisiasa itakuwa sawa sawia na hivyo kuwa kichocheo cha maendeleo ndani ya taifa.

Ni vema kuwa na mawazo mchanganyiko katika shughuli za kisiasa kuliko hoja za upande mmoja. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antoni Guterres anaamini "ufanisi katika uwepo wa kupingana kwa kutoa mawazo na fikira tofauti."

Mifumo ya utawala wa Rais Samia inazungumzia Watanzania wategemee uchaguzi wa haki, huru na wenye uwazi zaidi, vitu ambavyo vitawapa turufu ya ushindi vyama vya upinzani.

Japo wapo wahafidhina wasiokubaliana na namna serikali inavyowatendea wapinzani, wapo ambao wangefurahi Rais kuendelea kuwakaanga, lakini hakuna mamna sharti wakubaliane na mifumo ilivyo kwa sasa.

Rais wa awamu ya pili Ali Hassan Mwinyi, aliwahi kusema kila zama na kitabu chake, hivyo, ni vema wahafidhina wabadilike wakae kando kwa sasa wakati mifumo ya demokrasia na utawala bora ikiimarishwa.

Wapinzani wakubali turufu ya ushindi ipo mikononi mwa Rais Samia, naye amekubali, ni vema nyakati hizi vyama vikajenga mazoea ya kuwasilisha hoja zenye mashiko kwa jamii, kuepuka lugha chonganishi, hatarishi na isiyo na staha, ni vema upinzani ukarejea historia ya 'tulipotoka na tulipo kwa sasa.

Japo demokrasia si hisani lakini ni vema upinzani ukajisitiri ili na demokrasia iwasitiri pia.

***Maoni: 0717 718619***

JUKWAA LA VIONGOZI

## UCHAGUZI A/KUSINI 2024:

# ANC hoi, hatihati kuanguka




Mstaafu Jacob Zuma



Rais Cyril Ramaphosa wa ANC



Julius Malema wa EEF



John Steenhuisen wa DA

**Na Mwandishi Wetu**

WAAFRIKA Kusini wapo kwenye uchaguzi mkuu ulioanza mapema wiki hii. Wakati wakielekea kwenye boksi la kura baadhi ya ishara zinapendekeza chama tawala cha African National Congress (ANC) kinaweza kuanguka.

Kwa mujibu wa BBC kinaweza kupata chini ya asilimia 50 ya kura kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30.

Ukosoaji wa serikali ya ANC unaoongezeka dhidi ya chama kilichoongoza vita dhidi ya ubaguzi wa rangi chini ya hayati Nelson Mandela.

Hali hiyo imepunguza uungwaji mkono wake, na kuongeza uwezekano wa serikali ya mseto.

Leo karibu wapigakura milioni 28 wa Afrika Kusini waliojiandikisha wanachagua wawakilishi katika mabunge ya kitaifa na majimbo ambao ndiyo watakaomchagua rais ajaye.

Utakuwa uchaguzi mkuu wa saba wa kidemokrasia nchini humo tangu ANC ilipochukua uongozi na kwa mujibu wa katiba umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka mitano tangu 1994, wakati utawala wa weupe wachache ulipoisha na ANC kuingia madarakani.

### DALILI ANC CHALI

Chama cha ANC ambacho sasa kinaongozwa na Rais Cyril Ramaphosa, kinakabiliwa na shinikizo kubwa, inasema BBC.

Ukosefu wa ajira uliokithiri, ambao ulifikia asilimia 32 mwaka jana unatajwa. Aidha kukosekana kwa usawa wa kiuchumi, tuhuma za ufisadi na kukatwa pamoja na mgawo wa umeme mara kwa mara umepunguza umaarufu wake.

Viwango vya juu vya uhalifu wa kikatili, wastani wa ubakaji 130 na mauaji 80 kwa siku katika miezi mitatu iliyopita ya mwaka 2023 kadhalika yamepunguza imani kwa serikali na chama hicho.

Lakini ANC inasema inajitahidi kutatua matatizo haya, ikiwasihi watu wasifumbe macho kuona faida waliyopata tangu mwisho wa ubaguzi wa rangi, inaongeza B BC.

Chama hicho kinasema viwango vya umaskini vimepungua, idadi kubwa ya Waafrika Kusini wanaishi katika nyumba bora na upatikanaji wa huduma za afya umeboreka.

Chama cha ANC kimeahidi kutengeneza fursa mamilioni za kazi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ili kuimarisha uwekezaji, kusaidia sekta binafsi na kumaliza ufisadi.

### WAPINZANI DA, EFF

Chama kikuu cha upinzani cha Democratic Alliance (DA) kinasema "nchi iko kwenye mgogoro.' Kinataka kufanya uchumi huria, ikiwa ni pamoja na kuelekea kwenye ubinafsishaji mkubwa zaidi.

Kinaahidi kuongeza nafasi mpya za kazi 2,000,000 kumaliza kero ya kukatwa kwa umeme na "kupunguza kwa nusu kiwango cha uhalifu".

Ili kukabiliana na ukosefu wa ajira na usawa, Chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) cha tatu kwa ukubwa bungeni kina masuluhisho makubwa ya kiuchumi.

Kinahoji kuwa ANC haijarekebisha usawa wa kiuchumi wa ubaguzi wa rangi, aidha inapanga kugawa tena ardhi kwa watu walio na uwezo mdogo. EFF pia inaeleza nia ya kutaifisha migodi, benki na sehemu nyingine muhimu za uchumi, ikisema kwamba utajiri wa nchi hiyo utatumika kuwanufaisha watu wengi.

### ZUMA YUMO

Rais wa zamani, Jacob Zuma, ambaye aliondolewa madarakani na Ramaphosa kutokana na madai ya ufisadi ambayo anayakanusha na baadaye kufungwa jela kwa kukaidi amri ya mahakama, ameweka uzito wake wa kisiasa akiwa mpinzani mpya wa ANC.

Chama cha uMkhonto we Sizwe (MK), ambacho kimechukua jina lake kutoka kwa tawi la zamani la ANC, kinaongeza kutotabirika zaidi kufanya makubwa kwenye kinyang'anyiro hicho.

BBC inaeleza kuwa kinaweza kuwa na ushawishi mkubwa katika jimbo analotoka Zuma la KwaZulu-Natal na katika ilani fupi kinaahidi kubadilisha Afrika Kusini, ikiwa ni pamoja na lengo la kutengeneza nafasi za kazi 5,000,000.

Rais ajaye anaweza kuwa nani? Jibu ni kwamba Waafrika Kusini hawampigii kura rais.

Badala yake wanachagua wajumbe 400 wa Bunge la Kitaifa, ambao wanakwenda kumpigia kura kiongozi mpya wa nchi ndani ya siku 30 za uchaguzi mkuu.

Kwa hivyo, hakuna wagombea urais kama hao, lakini kila kiongozi wa chama anaongoza kampeni zao za kitaifa na picha yao itaonekana kwenye karatasi ya kura. Rais wa ANC Ramaphosa, John Steenhuisen wa DA na Julius Malema wa EFF wote watashiriki.

> Lakini ANC inasema inajitahidi kutatua matatizo haya, ikiwasihi watu wasifumbe macho kuona faida waliyopata tangu mwisho wa ubaguzi wa rangi, inaongeza B BC.

Kiongozi wa chama chochote anaweza kupata kura nyingi katika Bunge la Kitaifa baada ya uchaguzi atatarajiwa kuwa rais wa nchi hiyo. Katika uchaguzi wa 2024, wagombea wa kujitegemea watajumuishwa kwa mara ya kwanza.

### SERIKALI KITAIFA

Swali kwamba itaundwa vipi nchini Afrika Kusini, ni swali ambalo katiba haielezi jinsi muungano unavyoweza kuundwa.

Lakini kwa kuchukulia kuwa ANC inasalia kuwa chama kikubwa zaidi, makundi madogo madogo yanaweza kukubaliana kwa njia isiyo rasmi kuunga mkono serikali ya ANC kwa misingi ya kura baada ya kura ili kuingia katika makubaliano.

Aidha, kwa upande mwingine, ANC inaweza kuingia katika muungano rasmi na baadhi ya vyama, ikiwa ni pamoja na makubaliano ya maandishi yanayoelezea mipango ya kisheria na usambazaji wa nyadhifa za Baraza la Mawaziri.

Chama kingine chochote kitakabiliwa na chaguo sawa.

Lakini pia kuna uwezekano wa muungano wa upinzani. Katika mpango wa kabla ya uchaguzi, kundi la vyama, linaloongozwa na DA, limetia saini kile kinachojulikana kama Mkataba wa Vyama vingi vya Afrika Kusini, ikiwa kwa pamoja watapata zaidi ya asilimia 50 ya viti, tayari wamekubali kuunda serikali ya umoja, lakini mkataba huo haujumuishi Chama cha EFF cha Julius Malema, inaeleza BBC.





# Waziri awatwisha zigo mawakili mapambano ufisadi

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema mawakili wa serikali wanawajibu wa kuisaidia serikali kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka na mapambano dhidi ya ufisadi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo maalum kwa mawakili wa serikali yaliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali (AG).

Alisema mawakili wa serikali wana nafasi kubwa katika kuimarisha utawala bora kwa kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa serikali.

"Kusaidia kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka na kupambana na ufisadi kwa kuhakikisha kuwa sheria na taratibu zinafuatwa kikamilifu," alisema Simbachawene.

Aidha, alisema mawakili wa serikali wanajukumu la kulinda na kutetea maslahi ya umma kwa kuhakikisha kuwa haki inatendeka.

"Mnatekeleza hili kwa kutoa ushauri wa kisheria kwa serikali, kusimamia kesi za serikali na kuhakikisha kuwa shughuli zote za serikali zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria.

"Tatu mnakumbusha na kusisitiza umuhimu wa haki za binadamu na utawala wa sheria kupitia kazi yenu mnachangia katika kulinda haki za raia, kuhakikisha kuwa haki za msingi zinaheshimika na kwamba kila mtu anapata haki sawa mbele ya sheria," alisema.

Kadhalika, alisema mawakili wa serikali wanapaswa kusimamia haki za wananchi na serikali kwa ujumla.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuboresha utendaji kazi na kuwajengea uwezo mawakili wa serikali nchini.

Alisema: "Mafunzo haya yatakuwa ya siku sita na yatajumuisha mawakili wa serikali zaidi ya 200 ambao watajengewa uwezo masuala mbalimbali yakiwamo ya kitaaluma ili kuwasaidia kutoa huduma zao kwa weledi na ubora."



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma juzi. **PICHA: OWM**

## Samia aipiga 'tafu' TFS ujenzi vitalu vya miche

Na Paul Mabeja, DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameuwezesha Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), kujenga vitalu nyumba viwili vyenye uwezo wa kuzalisha miche zaidi ya milioni nane.

Lengo la ujenzi wa vitalu hivyo ni kusaidia kuendeleza juhudi za serikali kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi.

Meneja Msaidizi Raslimali Misitu kutoka TFS, Husna Msagati, alisema hayo jana wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuelezea mafanikio ya wakala huyo Mkoa wa Dodoma ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu, miti iliyozalishwa ni 3,505,756 ambayo ni wastani wa miche 1,168,586 kwa mwaka.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameiwezesha TFS kujenga bustani nne za kisasa ambazo zina uwezo wa kuzalisha miche milioni mbili kwa kila moja," alisema.

Alisema kuwa TFS imefanikiwa kupanda miti milioni tatu katika Mkoa wa Dodoma kupitia kampeni mbalimbali ikiwamo mti wa mama, soma na mti na kuhamasisha umma kupanda miti.

Alisema maeneo yalipopandwa ni pamoja na mji wa serikali Mtumba, barabara za mjini, maeneo ya wazi, kwenye shule na vyuo hususani Chuo cha Mipango.

Akizungumzia ongezeko la watalii wilayani Kondoa alisema TFS imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kuwa mazingira ya hifadhi yanakuwa bora ili kuweza kukuza utalii ikolojia na asilia.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewezesha serikali kupitia TFS kutekeleza kazi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba watalii wanaotembelea kituo hicho wanapata huduma bora.

## Vituo kuibua vipaji wenye mawazo kibiashara kuanzishwa

Na Renatha Msungu, DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuanzisha vituo kwa ajili ya kuibua vipaji vya vijana wenye mawazo ya kibiashara na bunifu, ili kuwasaidia kuondoa mikwamo ya kiuchumi inayowakabili.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Watu wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi aliyasema hayo wakati akizindua mtandao wa Taifa Letu, Kesho Yetu (TK Movement) hafla iliofanyika jijini hapa.

Alisema mtandao huo ni muhimu sana kama utatumika katika kuleta maendeleo kwa vijana kupitia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali.

Alisema asingependa kusikia mtandao huo unatumika kinyume na kile walichokisema wakati wa uzinduzi.

Alisema atafurahi kuona TK Movement inatumika kutafuta fursa za maendeleo.

Hata hivyo, alisema yuko tayari kuwatembelea TK Movement popote walipo endapo watamuhitaji kwa ajili ya fursa ambazo watakuwa wameziandaa.

Akizungumzia kuhusu uanzishwaji wa vituo hivyo alisema lengo ni kutaka kuwakwamua vijana katika biashara wanazofanya kupitia vituo hivyo ambavyo vitaanzishwa.

Pia aliwataka vijana kuchangamkia fursa ya mtandao huo ili waweze kupiga hatua badala ya kukaa vijiweni bila kazi yoyote.

Naye Waziri wa Madini, Antony Mavunde alisema sekta ya madini imeweka mkakati wa kubadilisha maisha ya Watanzania ikiwemo vijana ambao ni taifa la kesho.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema vijana wameamua kuungana kwa sababu wanalengo la kuendeleza dira, hivyo watumie mtandao huo kupeana fursa badala ya kupigana shoti.

Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ametekeleza miradi ya maendeleo kwa kasi hivyo ni vema vijana wakatumia fursa hizo.

# RC aziagiza h'shauri kupunguza vifo kinamama, watoto

Na Thobias Mwanakatwe, IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameziagiza halmashauri za wilaya mkoani hapa kuhakikisha zinaweka mikakati thabiti ya kupunguza au kuondoa tatizo la vifo vya kinamama na watoto kwenye vituo vya afya.

Alitoa agizo hilo juzi katika hutoba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda katika kikao kazi cha kujadili vifo vya kinamama na watoto wachanga vitokanavyo na uzazi.

Alisema ili kupunguza vifo vya kinamama na watoto madaktari katika halmashauri zote wanapaswa kutambua kuwa afya ya uzazi na mtoto ni suala la kimaendeleo, hivyo serikali inapambana kuhakikisha vifo hivyo vinapungua.

Alisema kila halmashauri inapaswa kuweka vipaumbele kwenye kamati kwa kujadili huduma ya mama na mtoto na kuimarishwa huduma kwenye ngazi ya jamii hususani kwenye kaya kabla ya kufika kwenye vituo vya huduma.

Alisema mkakati mwingine wa kupunguza vifo hivyo ni wajawazito kuwahi mapema katika vituo vya matibabu pale anapokuwa na changamoto za kiafya na ushiriki wa wanaume katika huduma za afya ya uzazi na mtoto ambalo ni jambo muhimu zaidi.

Aliongeza kuwa mkakati mwingine ni wajawazito kuwahi kliniki wanapohisi na rufani kwa wazazi ni jambo la kila mmoja.

"Halmashauri zisimamie mfumo wa M-mama kwa kuhakikisha magari ya wagonjwa yapo tayari wakati wote na kuhakikisha ushirikiano wa madereva jamii unakuwapo," alisema.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika kikao hicho wajawazito 155 wamefariki dunia katika kipindi cha kuanzia 2021 hadi 2023 katika Mkoa wa Singida.

Aidha, katika kipindi hicho watoto wachanga 1,820 wamefariki dunia na vizazi hai kuanzia Oktoba hadi Desemba 2023 na Januari hadi Machi 2024 vifo vya kinamama ni 33 na vifo vya watoto wachanga ni 285, huku vizazi hai ni 35,709.





# Wakulima mahindi Nyanda za Juu Kusini kuongeza uzalishaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mahindi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wanatarajiwa kuongeza tija ya uzalishaji kutoka gunia 15 mpaka 30 kwa ekari baada ya kuanza kutumia mbolea zenye mchanganyiko wa madini mbalimbali.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole imefanya utafiti katika mikoa hiyo na kubaini kuwa asilimia kubwa ya ardhi imeathirika kutokana na tindikali na hivyo ikaanza kutoa elimu kwa wakulima namna ya kurejesha madini yaliyopotea.

Mtafiti wa udongo wa taasisi hiyo, Fedrick Mlowe alisema ardhi ya mikoa hiyo imebainika kuwa na upungufu wa aina tano za madini ambayo ni muhimu kwenye uzalishaji wa mazao yakiwemo madini ya zink na boron.

Alisema kutokana na hali hiyo, tija ya uzalishaji ilikuwa hairidhishi hata kama wakulima watatumia mbolea na kwamba sasa wamefanya utafiti na kubaini kuwa ili kuongeza tija wakulima wanatakiwa kutumia mbolea zenye madini hayo.

Alisema mbali na upungufu wa madini hayo ya boron na zink, pia kwenye udongo wa mikoa hiyo kuna upungufu wa madini ya phosphate na sulfur ambayo ni muhimu kwenye uzalishaji.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Denis Tippe alisema waliamua kufanya utafiti huo baada ya kubaini kuwa tija ya uzalishaji wa mazao kwenye mikoa hiyo inashuka na kwamba kwenye baadhi ya vikao vya wadau wa kilimo, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alionyesha kukerwa na malalamiko ya wakulima.

Alisema waliamua kuanza kushughulikia kero za wananchi kwa kuanza kufanya utafiti wa afya ya udongo ili kubaini shida inayosababisha tija ya uzalishaji kushuka na kutafuta suluhu.

Alisema mbali na kupata suluhi hiyo ya kutumia mbolea zenye mchanganyiko wa madini muhimu, pia wanafanya utafiti na kuzalisha mbegu za kisasa za mazao mbalimbali yakiwemo ya chakula na biashara.

Dk. Tippe alisema kwa sasa wanawafundisha wakulima namna ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mahindi na kwamba baada ya hapo wataanza kuwafundisha mazao mengine ikiwemo mihogo.

Baadhi ya wakulima walioshiriki kwenye mafunzo hayo walisema kabla ya kupata mafunzo hayo walikuwa wanalima kilimo cha mazoea hali ambayo ilikuwa inawafanya wasipate tija inayokusudiwa.

Mmoja wa wakulima hao, Philemon Mbalale alisema walikuwa hawajui sababu ya uzalishaji kupungua na kwamba kwa sasa wameeleweshwa na wamepatiwa na mbinu za kukabiliana na tatizo hilo.



Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Mazingira Wizara ya Ujenzi, Mhandisi Mussa Kashinde (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mhandisi Jacob Mukasa (katikati) na Ofisa Mipango wa bodi hiyo, Pastory Ushidi, wakati alipotembelea Banda la Bodi hiyo, kwenye maonyesho ya Sekta ya Ujenzi, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Mil.348/- yamaliza kero ya maji Kijiji cha Sokoine

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANANCHI wa Kijiji cha Sokoine Ranchi wilayani Mvomero mkoani hapa wanatarajia kuondokana na adha ya kunywa maji kwenye mabwawa baada ya ujenzi wa mradi wa Sh. milioni 348 kuzinduliwa katika eneo hilo.

Wakizungumza na Nipashe wananchi wa kijiji hicho akiwemo Senyenda Olenaiko (69) alisema tangu ameanza kukaa kwenye kijiji hicho hawakuwahi kuwa na mabomba wala kutumia maji hadi mwaka huu walipoona wamewekewa matangi na vituo vya maji.

"Nimeishi kijiji hiki tangu mwaka 1970 hatujawahi kuyaona mabomba ya maji safi, kwa miaka yote tumekua tukitumia maji ya mabwawa na madimbwi ambayo tumeyatumia pamoja na mifugo, sisi tunakunywa humo na mifugo humo humo" alisema Olenaiko.

Alisema anaishukuru serikali kwa kusikia kilio na kuwasogezea huduma ya maji ambayo itawafanya kuwa na uhakika wa kuwa na afya bora kwa sababu maji safi na salama huwaepusha na magonjwa.

Naye Raheli Seperali alisema ujenzi wa mradi huo utawasaidia kupunguza au kuondoa kabisa adha ya kuamka asubuhi sana kufuata maji kwenye mabwawa kabla mifugo haijaelekezwa bwawani kunywa maji ili waweze kupata maji safi ya kutumia.

Naye Mbunge wa Mvomero, Jonas Van-Zeeland alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa miradi mingi ya maji jimboni humo ikiwemo kulifikia eneo hilo ambalo lilikuwa na changamoto kubwa sana ya maji.

Hata hivyo, aliiomba serikali kuona umuhimu wa kutumia chanzo cha maji Dakawa kupeleka maji kwenye vitongoji vya Mkambarani na Kwa Wagogo ambavyo havina maji.

Akizungumza mara baada ya kuzindua ujenzi wa mradi huo, Naibu Waziri wa Maji, Kundo Matwew aliwataka wananchi wenye malengo ya kupata huduma za maji majumbani kuwasilisha maombi MORUWASA ili kupata huduma hiyo ndani ya siku saba.

Alisema mradi huo uliasisiwa na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso aliposhuhudia wananchi wakichota maji machafu waliyochangia na ng'ombe.

Alisema ujenzi wa mtandao wa vituo vya maji 12 (DP) unatarajiwa kukamilika Juni mwaka huu, ukihusisha ujenzi wa tangi la maji lenye ujazo wa lita 50,000 na mtambo wa kusafirishia maji hayo.

Katika hatua nyingine akiwa katika Kijiji cha Kichangani wilayani Mvomero, Naibu Waziri huyo aliitaka Mamlaka ya Maji Turiani (TURUWASA) kupeleka mapendekezo Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ili kupata tathmini mpya ya gharama za huduma za maji.

Alitoa agizo hilo baada ya wananchi wa eneo hilo kulalamikia kupata bili kubwa za maji tofauti na matumizi yao.

# Miaka 16 wosia 1,350 imeandikwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KATIKA kipindi cha mwaka 2008 hadi sasa idadi ya wosia iliyoandikwa ni 1,350, hali inayoonyesha bado kuna tatizo la uwoga wa kuandika wosia.

Hivyo, watanzania wametakiwa kujenga utamaduni wa kuandika wosia ili kuepuka migogoro ya kifamilia ambayo inasababishwa na wanafamilia kugombea mali za marehemu.

Ushauri huo ulitolewa na Wakili wa Serikali kutoka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Janeth Mandawa wakati akitoa elimu kwenye kampeni ya msaada wa sheria inayofanyika mkoani hapa.

Alisema kiasi hicho ni kidogo hivyo wapo kwenye jitihada za kubadilisha mtazamo kwa watanzania kuacha kuona wosia ni uchuro na badala yake waone ni suala la uwajibikaji katika familia.

"Lakini vilevile unapoamua kuandika wosia, wosia unaouacha kwa namna yeyote unayopenda hakuna kusema mpaka uwe na mali nyingi sana, hiyo mali moja inaweza kuleta mtafaruku," alisema Mandawa.

Alisema suala zima la uandishi wa wosio lina mtazamo hasi kwa sababu wengi wanaamini kwamba kuandika ni kujichulia kufa na hivyo wamekuwa wakilikimbia.

Mandawa alisema ili kuongeza idadi ya watu wanaoacha wosia na kupunguza migogoro ya kimirathi wakala huo umekuwa ukitoa elimu kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari.

Baadhi ya wananchi mjini Njombe wamesema hawana elimu sahihi juu ya uandishi wa wosia jambo ambalo linasababisha matatizo kwenye familia ikiwemo mauaji.

Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal Aid kwa siku 10 inaendelea katika wilaya sita mkoani hapa ikiwa na lengo la kusaidia wananchi wasio kuwa na uwezo wa kulipa mawakili kupata huduma hiyo bure bila ya malipo.

# Mama lishe 100 kupewa mitaji kukuza biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMA lishe zaidi ya 100 wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatarajiwa kunufaika na msaada wa mtaji utakaowasaidia kuboresha huduma zao na kukuza biashara.

Mtaji huo unatarajiwa kutolewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela.

Mwaselela aliahidi kugawa mtaji huo juzi alipofanya kikao na vijana wenye taaluma mbalimbali katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kwa ajili ya kusikiliza kero zao.

Alisema mtaji huo unatokana na faida ambayo anapata kutokana na uwekezaji wake kwenye shule zake za Patrick Mission iliyopo jijini Dar es salaam na Paradise Mission iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya.

Alisema msaada huo atagawa bila kujali itikadi za kisiasa wala ubaguzi wa aina yoyote na badala yake kuna vigezo vitaandaliwa vya kuwashindanisha mama lishe hao.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Kenneth Laulesi alisema mikutano ya kusikiliza kero za wananchi inayofanywa na viongozi wa chama hicho mbali na kutatua kero hizo pia inasaidia kuwaunganisha wananchi.

Hivyo, aliwataka vijana kufanya kazi kwa bidi ili kujiletea maendeleo, huku akisisitiza kwamba Mkoa wa Mbeya una fursa nyingi za kiuchumi ambazo vijana wakizichangamkia wanaweza kupata utajiri.



# Idadi wasichana wanaopata VVU Zanzibar yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya idadi ya watu wanaopata maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kupungua visiwani Zanzibar, lakini bado kuna changamoto kwa vijana wa kike (15-24) kupata maambukizi mapya, kwamba idadi yao inaongezeka.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Tume ya UKIMWI Zanzibar, Dk. Ahmed Mohamed Khatib, wakati akizungumza na wadau wa kupambana na maambukizi ya VVU Zanzibar.

Alisema kwa sasa maambukizi mapya ya virusi hivyo yamepunguwa na watu 60,000 wanapata maambukizi hayo kwa mwaka tofauti na miaka ya nyuma ambapo kila mwaka watu 72,000 walikuwa wakipata maambukizi.

Alisema jitihada kubwa zinahitaji kufanyika kwa vijana wa kike wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24, ambapo kundi hilo lipo juu kwa kuwa na maambukizi mapya ili kupunguza maambukizi ya VVU.

Mkurugenzi huyo alisema miongoni mwa vitu vinavyochangia maambukizi makubwa kwa kundi hilo la wanawake vijana ni udhalilishaji wa kijinsia kwa sababu utafiti unaonesha kwamba vijana wa kike wenye umri huo watatu kati ya 10 wanadhalilishwa.

Aidha, alisema mkoa unaongoza kwa kuwa na maambukizi ya VVU ni Kusini Unguja ambao una asilimia 0.8 ikilinganishwa na mikoa mengine visiwani Zanzibar, kwamba asilimia ya maambukizi kwa watu wote wa Zanzibar ni 0.4.

Alisema tatizo la UKIMWI Zanzibar lipo zaidi katika makundi maalum matatu wakiwamo wanawake wanaofanya biashara ya kuuza mwili, wanaume wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja na vijana wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunda sindano.

Alisema katika utafiti wa mwisho uliofanyika mwaka 2007, wanawake wanaouza miili yao wana asilimia 21.1 ya VVU, wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja ni asilimia 11.4 na vijana wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano ni asilimia 9.3.

Naye Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, Hassan Ibrahim Suleiman, alitaka jamii kuwa na malezi na makuzi ya ushirikishwaji, ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji ambavyo vinachangia athari mbalimbali ikiwamo maambukizi ya VVU.

Alisema malezi ya mzazi mmoja yanachangia kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji na mzigo mkubwa wa malezi ya watoto huachiwa mama.

Alisema misuli ya nidhamu inatengenezwa na baba katika familia, hivyo watoto wengi wanaokosa malezi ya baba na wanaweza kupata shida baadaye katika kuhimili mikiki ya maisha.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo, walisema elimu zaidi inahitajika kwa vijana ili kupunguza maambukizi ya VVU.

Pia, waliitaka serikali kuifungia mitandao ya kijamii inayohamasisha mambo maovu ikiwamo mapenzi, kwamba vijana wengi hujifunza kupitia mitandao hiyo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Huduma za fedha kupitia simu zaleta mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamed Mussa, amesema huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zimeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya fedha visiwani Zanzibar.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa huduma ya lipa ada ya shule kwa njia ya teknolojia ya mawasiliano mtandaoni.

Alisema huduma hiyo ni suluhisho la kipekee linalolenga kuboresha na kurahisisha malipo ya ada za shule.

Leila alisema katika dunia ya sasa ambapo muda ni rasilimali adimu ni muhimu kuwa na mifumo inayowezesha malipo kufanyika kwa haraka, kwa usalama, na kwa urahisi zaidi.

"Nimesikia kupitia huduma hii, wazazi na walezi wataweza kulipa ada za shule kwa njia ya simu za mkononi, hivyo kuokoa muda na gharama za kusafiri kwenda benki au ofisini. Hii itasaidia pia kupunguza msongamano wa watu kwenye taasisi za kifedha na kuongeza ufanisi wa malipo kwa ujumla," alisema waziri huyo.

Aidha, alisema teknolojia inabadilika kwa kasi na ni jukumu la kila mtu kuhakikisha kuitumia kuboresha maisha ya wananchi.

Alisema huduma ya lipa ada siyo tu kwamba inarahisisha maisha ya watu, bali pia inachangia katika kujenga jamii yenye maarifa zaidi kwa kurahisisha upatikanaji wa elimu.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya ZMOTION, Said Hemed Ali, alisema huduma hiyo imelenga kusaidia shule katika usimamizi wa fedha na taarifa za kitaaluma kwa kutumia miundombinu ya kiusalama katika kuchakata miamala.

Alisema mfumo huo pia utasaidia kupima ufanisi wa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao kwa kuchataka matokeo yao na kufahamu mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

# Miradi ya kimkakati kujengwa maeneo ya kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif, amesema serikali imejipanga kutekeleza miradi ya kimkakati katika maeneo huru ya kiuchumi, ikiwamo ujenzi wa viwanda ambavyo vitaongeza ajira na uzalishaji.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari baada ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2024-2025.

Alisema miongoni mwa mikakati hiyo ni kukifungua Kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji kwa kuimarisha maeneo huru ya uchumi yaliopo Micheweni pamoja na kutekeleza miradi ya kimkakati itakayoongeza pato la taifa.

Sharif alisema kazi kubwa ambayo imekamilika katika maeneo huru ya uchumi yaliopo Pemba ni kufikishwa kwa huduma za miundombinu ya barabara pamoja na maji na umeme.

Alisema serikali imefanikiwa kufikisha miundombinu ya ujenzi wa barabara katika maeneo huru ya uchumi Micheweni yenye urefu wa kilomita 13.5 yenye thamani ya Sh.bilioni 2.93.

Aidha, alisema serikali imejipanga kuweka mazingira mazuri katika upatikanaji wa ajira katika sekta binafsi ambazo zitakuwa za staha.

Alisema upatikanaji wa ajira rasmi za ndani umeimarika kwa asilimia 65.9 kutokana na mikataba iliyothibitishwa kutoka ajira 6,348 katika mwaka 2022-2023 hadi ajira 9,630 mwaka 2023-2024 katika sekta binafsi ikiwamo hoteli za kitalii.

Waziri huyo alisema usajili wa miradi 63 ya uwekezaji yenye hadhi ya mitaji mikubwa yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,499 imeidhinishwa ambayo inatarajiwa kutoa ajira zipatazo 4,392.

Alisema tayari miradi 12 imefunguliwa na mingine kuwekewa mawe ya msingi katika kipindi cha maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema matumaini makubwa ya kuongezeka kwa uwekezaji yamekuja baada ya kusainiwa Sheria ya Uwekezaji Namba 10 ya Mwaka 2023 ambayo ni miongoni mwa sheria bora zenye kuweka mikakati katika sekta ya uwekezaji na kuifanya Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kuwa kituo bora cha uwekezaji Afrika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALIM A. SILIM** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **T131-0120,** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NGUVUMALI SECONDARY SCHOOL** mwaka **1973.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/100060/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FABIAN J. YADALALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S2096-0034.** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **USULE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016, Cheti hiki kimepotea mkoani Shinyanga. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KAU/RB/2194/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RAMADHAN HASSAN NKUSA**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari Mitsubishi yenye namba za usajili **T 568 ASS.** CHASSIS NO **FE637EV520689** NA ENGINE NO **4D33E40772**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/KIL/HAI/ 10803/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SAUKO PILULA TIMOTH**

anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 655 AUG** na **MC 730 BHS,** CHASSIS NAMBA: **MD2A21BZ2FWC72861 na MD2A21BZ0GWB89740** na ENGINE NAMBA: **PFZWFC76303 na PFZWGB71696.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/99288/2024**

**PHQ/DAR/KIN/99322/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OLIVER RISHAELY KAAYA,**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **TOYOTA PREMIO** yenye namba za Usajili **T 602 DHW,** CHASSIS NAMBA **NZT2405006998,** ENGINE NAMBA **1NZA758731,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/DOD/DOD/20587/2024**

## ENEO LINAUZWA

**ENEO LENYE UKUBWA WA 26,950SQM LINAUZWA** LIMEPAKANA NA BARABARA INAYOELEKEA KIWANDA CHA KIOO LTD LIPO VIANZI, **WILAYA YA MKURANGA.** WAWEKEZAJI WOTE WANAKARIBISHWA, NA BEI NI MAELEWANO (NECOTIABLE) KWA MWENYE KULIHITAJI APIGE SIMU ZIFUATAZO::-

**0786 641903, 0716 172929**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA GARI

**LOVENESS KARIA MGONJA**

anatangaza kupotea kwa kadi za gari zenye usajili namba **T 247 AVB na T121 BAG** zenye CHASSIS NAMBA: **BW4002012** na **NKR58E7405079** na kadi za pikipiki zenye usajili namba **T 667 CDH na T863 CDJ** zenye CHASSIS NAMBA: **LDAPAJ0B0CGB13307 na LDAPAJ0B8CGB13278.** Kwa yeyote atakaezikona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/100379/2024**

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 10039 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the Late DAN ELFOARD MATEKERE**

**And**

**In the matter of Application for letters of administration by SAMUEL DAN MATEKERE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above –named deceased are hereby cited to come and see proceedings if they think fit before the grant of probate( or letters of administration)is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **17th day of JUNE 2024**

Dated at DAR ES SALAAM this **6th day of MAY 2024**

Principal Resident Magistrate

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 271/272 YA 2023**

**NYANZA CO-OPERATIVE UNION 1984 LTD ............ MDAI**

**DHIDI YA**

**ABDUL QUABID ALLY ABDALLAH .................. MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI.**

**KWA; ABDUL QUABID ALLY ABDALLAH. POPOTE ULIPO**

**NYANZA CO-OPERATIVE UNION 1984 LTD.** amefungua Shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Temeke. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 29/05/2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya **MH. L. R. RUGARABAMU,** Mwenyekiti wa Baraza.

Unatakiwa ufike wewe au wakili wako au mwakilishi wako pasipo kukosa.

AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 14 mwezi 05, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA TEMEKE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 12287 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late RISPA CHRISTOPHER MASHAURI of NKUHUNGU WARD Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SAULI STEVEN NDEJEPA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 24 Day of June, 2024

Dated at Dodoma this **20th Day of May, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**THE UNITD REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT COUNCIL OF MBEYA**
**AT MBEYA**

**CRIMINAL APPEAL NO. 8553/2024**

**ANNA MOHAMED...........APPELLANT**

**VERSUS**

**SELEMAN SIMON............RESPONDENT**

**TO: SELEMAN SIMON**

**WHEREVER YOU ARE.**

Take note that,Appellant filed an appeal against you on 17/04/2024 in the District Magistrate Court of Mbeya at Mbeya,so you are ordered to appear before this court either yourself or your advocate on 31/05/2024,at 08:00 in the morning.
Understand that,if you fail to appear on that day,the matter will be heard ex-parte and the decision will be made ex-parte.

**Issued on 20th day of May,2024.**

**Order accordingly.**
**RESIDENT MAGISTRATE**
**MBEYA.**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUS-TRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

HABARI KIMATAIFA

# Baraza la usalama laitisha kikao dharura kujadili Rafah

**GAZA,** PALESTINA

BARAZA la Usalama limeitisha kikao cha dharura kujadili Israel inayoendelea kukumbwa na wimbi la shutuma kutoka jumuiya ya kimataifa kuhusiana na shambulizi lake ambalo maofisa wa Gaza wamesema liliwauwa watu 45.

Inaelezwa kuwa shambulizi hilo lilisababisha moto mkubwa katika kambi ya wakimbizi wa Kipalestina. Huku Israel kupitia Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu ikisema inachunguza tukio hilo ililoliita ajali ya kusikitisha na athari zake kwa raia.

Jeshi la Israel lilisema shambulizi hilo la Jumapili usiku kusini mwa Rafah liliwalenga na kuwauwa maofisa wawili waandamizi wa Hamas lakini pia likasababisha moto ambao Wapalestina na nchi nyingi za Kiarabu zimelaani kwa kuliita tukio hilo mauaji ya kikatili.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Marekani alisema Israel lazima ichukue tahadhari zote kuwalinda raia. Huku Mjumbe wa Umoja wa Mataifa katika Mashariki ya Kati Tor Wennesland akiitaka Israel kufanya uchunguzi wa kina na wa wazi kuhusu tukio hilo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres alilaani shambulizi hilo akisema liliwalenga raia wasio na hatia ambao walikuwa wametafuta hifadhi kutokana na vita vinavyoendelea, akieleza kuwa hakuna mahali salama katika Ukanda wa Gaza na kusisitiza kwamba ukatili huo lazima ukomeshwe.

Aidha, Mawaziri wa mambo ya kigeni wa Umoja wa Ulaya wamekubaliana kufanya mkutano wa Baraza la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya na Israel ili kutathmini uzingatiaji wa Israel wa makubaliano ya jumuiya hiyo ya wajibu wa haki za binadamu.

Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borell, alitangaza hatua hiyo mjini Brussels wakati akiongeza shinikizo dhidi ya Israel kutii uamuzi kutoka Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) na kusitisha mashambulizi yake katika mji wa Rafah, kusini mwa Gaza.

Borell alisema inakwenda kinyume na uamuzi wa ICJ, kwa kuongeza shughuli zake za kijeshi, mashambulizi ya mabomu na kuongezeka kwa idadi ya raia wanaouawa na kujeruhiwa.

Mkuu huyo wa sera za kigeni alisema mawaziri wa mambo ya kigeni wamemtaka apendekeze hatua nyingine zaidi kuhakikisha Israel inatii uamuzi wa ICJ.

Umoja wa Ulaya umeendelea kulaani mashambulizi ya kigaidi ya Hamas ya Oktoba 7 nchini Israel ambayo yaliwauwa zaidi ya watu 1,200 na watu 250 kuchukuliwa mateka lakini ukosoaji wa namna Israel inavyoshambulia Gaza umekuwa ukiongezeka.

Mawaziri wa Umoja wa Ulaya pia walifanya mazungumzo yasiyo rasmi na mawaziri wenzao kutoka Saudi Arabia, Jordan, Misri, Umoja wa Falme za Kiarabu na Qatar, pamoja na katibu mkuu wa Mataifa ya Jumuiya ya Kiarabu.

Baada ya mkutano huo, Borell alisema mawaziri kutoka mataifa ya Kiarabu walipendekeza kufanyika kongamano la kimataifa la kutekelezwa kwa suluhisho la mataifa mawili kwa mgogoro wa Israel na Hamas.

*DW*



Wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wakiwa katika kikao cha dharura kujadili shambulizi la Rafah jana.
**PICHA: DW**

# Guterres: Changamoto za ulimwengu zinaongezeka afya ikizorota

**NEW YORK,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres amesema changamoto za ulimwengu zinaongezeka huku afya za watu zikizidi kuzorota kutokana na mamilioni ya raia Sudan na Gaza kuwa hatarini kufa sio tu kutokana na risasi na mabomu lakini majeraha yasiyotibiwa na magonjwa.

Baraza Kuu la 77 la Shirika Afya Duniani (WHO) lilifungua kikao chake cha kila mwaka, wakati wajumbe wakiwa wanakabiliwa na jukumu la kuweka sera za afya kwa mwaka ujao huku kukiwa na changamoto kubwa kwa ustawi wa ulimwengu kutokana na migogoro mingi ambayo, katika baadhi ya maeneo, ilitishia kufuta miongo kadhaa ya maendeleo.

Aidha, Guterres aliliambia baraza hilo kwa njia ya video kutoka New York nchini Marekani, kwamba dunia inakabiliwa na matatizo na kwamba afya ya ulimwengu inataabika "kuanzia machafuko ya hali ya hewa hadi kuongezeka kwa umaskini na ukosefu wa usawa, na kuzidisha migogoro".

Alisema zaidi ya watoto milioni 20 wanakosa chanjo za kawaida, kwamba homa za msimu au dengue, na magonjwa mengine yanaongezeka kutokana na kuongezeka kwa joto duniani, pamoja na milipuko ya kipindupindu ambayo imetokea katika nchi zaidi ya 20 mwaka huu pekee.

"Mashambulizi yasiyo ya kawaida dhidi ya vituo vinavyotoa huduma za afya huenda ikawa ni zaidi ya kitu chochote ambacho nimeshuhudia katika wakati wangu kama katibu mkuu," alisema Guterres.

*VOA*

## Wanigeria wajificha wakihofia kutekwa nyara

**ABUJA,** NIGERIA

WALIONUSURIKA katika tukio la utekaji nyara wa watu kaskazini mwa Nigeria wamesema wanahofia maisha yao, baada ya wananchi 10 kuuawa na wengine 160, wengi wao wanawake na watoto, kutekwa nyara Ijumaa iliyopita katika kijiji cha Kuchi katika jimbo la Niger.

Mkazi mmoja aliiambia BBC jana kwamba watu sasa wanajificha vichakani, baada ya wavamizi wengine kurejea Jumapili usiku.

„Nina huzuni. Inasikitisha sana. Wakati wowote wanaweza kurudi. Watu waliobaki wanajaribu kujificha vichakani," alisema mkazi huyo.

Kamishna wa Usalama wa Ndani wa Jimbo la Niger, Muhammed Bello, alisema idara yake, pamoja na vyombo mbalimbali vya usalama, vinachunguza utekaji nyara huo, ingawa amepinga idadi ya watu waliochukuliwa.

"Kwa kweli haimaanishi kwamba wote wamechukuliwa na waasi au majambazi, baadhi yao huenda wamekimbilia msituni au kuvuka maji kwa sababu ya mkanganyiko," alisema.

Kamishna huyo aliongeza kuwa serikali inafanyia kazi mpango wa mashirika mbalimbali ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya mashambulizi.

"Tunashirikiana kwa hivyo tuna operesheni hizi za kijeshi zinazofanyika katika majimbo kwa wakati mmoja, kwa hivyo hakutakuwa na njia ya kutoroka kwa yeyote kati yao," alisema.

Hata hivyo, wakosoaji wanaishtumu serikali kwa kushindwa kuzuia mashambulizi, ambayo yamekithiri katika majimbo ya kaskazini.

Akiongea kwa niaba ya mgombea urais wa chama cha Labour Peter Obi, Dk. Yunusa Tanko alisema ongezeko la idadi ya utekaji nyara katika maeneo fulani ni la kushangaza, kwa sababu ya kile alichoeleza kuwa kupuuzwa kwa serikali za mitaa katika maeneo ya mashambani.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Amnesty International lilisema lina wasiwasi mkubwa juu ya utekaji nyara wa watu wengi, likisema ni dalili nyingine ya kushindwa kabisa kwa mamlaka ya Nigeria kulinda maisha.

Katika kipindi cha mwezi uliopita, vijiji kadhaa vimevamiwa na magenge yenye silaha ambayo yanawateka nyara ili kujipatia fidia.

Mara nyingi haijulikani ikiwa watu hao wenye silaha wana uhusiano wowote na makundi ya kijihadi.

*BBC*

## Mlandege FC yajiweka pazuri kubaki Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

USHINDI wa bao 1-0 walioupata juzi dhidi ya Maafande wa Hard Rock kwenye mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar umeifanya Mlandege FC kuwa kujiweka katika mazingira mazuri ya kubaki kwenye Ligi hiyo msimu ujao.

Mchezo wa juzi ulikuwa muhimu kwa timu zote kutokana na nafasi zao kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoenda ukingoni.

Matokeo ya juzi yameifanya Hard Rock kuwa katika mazingira magumu zaidi kuendelea kubaki Ligi kuu.

Mchezo huo ambao ulikuwa wa kuvutia licha ya kuhudhuriwa na mashabiki wachache kwa timu zote mbili, umeifanya Mlandege kupanda mpaka nafasi ya nane huku Hard Rock Fc wakibaki nafasi ya 10.

**Mlandege sasa imefikia pointi 36 huku Hard Rock wakibaki na pointi zao 30. Akizungumza na gazeti hili, Kocha wa Mlandege FC, Hassan Ramadhani alisema licha ya kutoka katika nafasi za chini kabisa lakini bado malengo yao yapo katika kushinda michezo minne ili yobakia.**

Alisema bado Ligi inaendelea licha ya ugumu wake lakini watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwenye michezo minne iliyobaki.

"Tumeshinda mchezo huu ambao ulikuwa mgumu, lakini tunamatumaini ya kushinda michezo mingine iliyobakia ili kuwa katika nafasi za juu zaidi katika msimamo wa Ligi ", alisema Ramadhani.

Katika mchezo mwingine wa juzi, kwenye uwanja wa Amaan, Mafunzo FC walifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Chipukizi FC.

Matokeo hayo yanaifanya Mafunzo FC kupanda mpaka nafasi ya tano kwa kukusanya pointi 41 wakati Chipukizi FC ikibaki nafasi ya saba kwa kuwa na pointi 38.

Kikundi cha ngoma za asili cha Wazalendo Culture, kikitumbuiza kwa wageni waliohudhuria kwenye uzinduzi wa pikipiki mpya katika hafla iliyofanyika jijini Dar as Salaam juzi. PICHA: MIRAJI MSALA



# AZAM FC YASHUSHA MRITHI WA PRINCE DUBE CHAMAZI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kusajili wachezaji watatu mpaka sasa kabla ya kuanza kwa msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa, inaelezwa klabu ya Azam imekamilisha usajili wa mshambuliaji, Jhonier Alfonso Blanco, raia wa Colombia, akitokea kwenye klabu ya Rionegro Aguilas ya nchini humo.

Inaelezwa nyota huyo tayari amemalizana na Azam na muda wowote matajiri hao watamtangaza ikiwa ni siku chache baada ya kumtangaza kiungo mkabaji, Ever Meza kutoka klabu ya Leonnes FC ya huko huko Colombia.

Mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo amesema straika huyo anaweza kutambulishwa wakati wowote kuanzia sasa, baada ya kila kitu kukamilika, ikiwa ni pamoja na kupata vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini.

„Huyu pia ni Mcolombia, tumeamua kwenda Amerika ya Kusini, kule kuna wachezaji wenye vipaji sana, wanaoweza kucheza katika mazingira ya huku kwetu bila matatizo yoyote kwa sababu mazingira yetu na huko kwao yanafanana kwa kiasi kikubwa, wanajituma, waaminifu na si wasumbufu, ili mradi tu unawatekelezea matakwa yao," kilisema chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 23, ndiye anayetajwa kuja kuchukua nafasi ya Prince Dube ambaye kwa kipindi kirefu cha mzunguko wa pili wa Ligi Kuu hakuwa uwanjani kutokana na kuzuka mgogoro wa kimkataba baina yake na waajiri wake.



Wakati Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24, ikiwa imemalizika jana, tayari Azam imeonekana kumaliza mapema biashara ya kusajili, kwani tayari imeshawatangaza rasmi wachezaji watatu.

Mbali na Meza, imemsajili beki wa kati Yoro Mamadou Diaby kutoka klabu ya Stade Malien de Bamako ya nchini Mali, pamoja na kiungo mshambuliaji kutoka timu hiyo hiyo, Franck Tiesse.

**SOKA**

## NUSU FAINALI FA Z'BAR KUPIGWA LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MICHEZO ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) imepangwa kuchezwa leo kwenye viwanja vya Mau A na Mau B.

Katika uwanja wa Mau B, Mlandege FC itacheza na Uhamiaji FC wakati katika Uwanja wa Mau B, Maafande wa Zimamoto SC watavaana na JKU SC huku michezo yote ikipangwa kuchezwa muda mmoja, saa 10:00 Alasiri.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa timu hiyo Mohamed Hilali 'Tedy', alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu lakini wamejiandaa kuhakikisha wanavuka hatua hiyo.

Alisema lengo kubwa kwa timu yake msimu huu ni kuhakikisha anashinda mataji yote mawili, Ligi Kuu na Kombe la FA hivyo watajitahidi kuhakikisha lengo lao linatimia.

Alisema katika mchezo huo atatumia mbinu ambayo itaweza kufanikisha kupata matokeo ambayo yataipeleka timu hiyo fainali.

Aidha alisema, anawafamu wapinzani wake kutokana uwezo wao mkubwa hasa katika msimu huu ambao wanafanya vizuri katika Ligi kuu ya Zanzibar hivyo lazima aingie uwanjani kwa tahadhari.

"Tunashuka uwanjani tukiwa tunajua kwamba Tunacheza na timu ambayo ndio kinara wa Ligi kuu, lakini tunacheza na timu ambayo ina malengo sawa na sisi katika michuano hii, hivyo lazima wachezaji wajue kama tunamchezo mgumu na lengo letu ni kusonga mbele"Alisema.

Hata hivyo alisema kuwa katika mchezo huo atamkosa mshambuliaji wake, Hamad Hilika ambae amejiunga na kikosi cha timu ya taifa ya Tanzania ,Taifa Stars'.

## ZISIKUPITE

### ZEBRI AHUSISHWA MAN U

MANCHESTER United wamezungumza na kocha wa zamani wa Brighton, Roberto de Zerbi kuhusu uwezekano wa kumrithi Erik ten Hag kama kocha. ***(Guardian)***

### MCKENNA AKARIBIA KUSAINI

KOCHA wa Ipswich Kieran McKenna anakaribia kusaini mkataba mpya wa kudumu licha ya Chelsea, Manchester United na Brighton kumtaka. ***(Athletic)***

### BRUNO GUIMARAES AGOMBEWA

KLABU ya Paris St-Germain wako tayari kuchuana na Manchester City na Arsenal kumwania kiungo wa kati wa Newcastle na Brazil, Bruno Guimaraes, 26, mwenye thamani ya pauni milioni 100. ***(Goal)***

### LALLANA KUREJEA SOUTHAMPTON

KIUNGO wa kati wa zamani wa England Adam Lallana mwenye miaka 36, yuko kwenye mazungumzo ya kurejea Southampton kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake wa Brighton utakapokamilika mwezi ujao. ***(Telegraph)***

### ADARABIOYO ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inafikiria kumenyana na Newcastle kumnunua mlinzi wa Uingereza Tosin Adarabioyo mwenye miaka 26, ambaye atakuwa mchezaji huru mkataba wake utakapokamilika Fulham mwezi ujao. ***(The i)***

### FRASER AWANIWA

KLABU ya Southampton itajaribu kuwasajili winga wa West Ham Muingereza Flynn Downes mwenye umri wa miaka 25, na winga wa Newcastle wa Scotland, Ryan Fraser mwenye umri wa miaka 30 kwa mikataba ya kudumu baada ya kucheza kwa mkopo msimu uliopita. ***(Daily Echo)***

### CORBERAN ATAJWA BROM

LEICESTER City huenda wakamlenga Kocha wa West Brom, Carlos Corberan iwapo Enzo Maresca atajiunga na Chelsea. ***(Talksport)***

### TRAFFORD ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United wanafikiria kuwasilisha dau la pauni milioni 20 kumnunua mlinda mlango wa Burnley mwenye miaka 21 raia wa Uingereza James Trafford. ***(Mail)***

### LIVERPOOL PIA INAMTAKA

LIVERPOOL pia inamtaka James Trafford, huku kipa wao wa Jamhuri ya Ireland Caoimhin Kelleher mwenye miaka 25 akijiandaa kuondoka katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### CASEMIRO HUYO SAUDIA

KLABU ya Manchester United inatarajia kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye miaka 32, kujiunga na klabu ya Ligi Kuu ya Saudia katika msimu huu wa majira ya joto na wako tayari kumuuza. ***(Football Insider)***



# RONALDO AVUNJA REKODI SAUDIA

**●●●Nyota huyo atamba kuwa hafuati rekodi bali rekodi zinamfuata na ndio sababu ya...**

**RIYADH,** SAUDI ARABIA

MCHEZAJI wa Al Nassr, Cristiano Ronaldo amemaliza msimu wake wa kwanza wa Ligi ya Saudi Arabia kwa kuvunja rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 alifunga mabao mawili katika ushindi wa 4-2 wa timu yake dhidi ya Al Ittihad siku ya mwisho ya mechi na kufikisha jumla ya mabao 35 katika ligi msimu huu.

Ronaldo aliandika kwenye Instagram: „Sifuati rekodi, rekodi zinanifuata," na katika mahojiano na SSC aliongeza: „Nina furaha sana. Kwanza kwa sababu timu ilishinda na kumaliza ligi vizuri. Kisha kuvunja rekodi ya mabao ya ligi, lazima nikiri inanifurahisha sana, sikuitarajia.

„Kwangu mimi ni muhimu. „Jambo muhimu zaidi ni timu kila wakati. Tuko katika hali nzuri. Tulimaliza ligi vizuri."

Rekodi ya awali ilikuwa ikishikiliwa na mshambuliaji wa zamani wa Al Nassr na mchezaji wa kimataifa wa Morocco, Abderrazak Hamdallah, ambaye alifunga mabao 34 msimu wa 2018-19.

Ronaldo, ambaye aliichezea Sporting, Manchester United, Real Madrid na Juventus, alijiunga na Al Nassr Januari 2023.

Katika sekunde za mwisho za kipindi cha kwanza, Ronaldo, ambaye tayari alikuwa amefunga mabao mawili yaliyokataliwa kwa kuotea, alifunga akiunganisha pasi ndefu kutoka kwa Mohammed Al-Fatil na kufungua ukurasa wa mabao kwa shuti hafifu kutoka upande wa kushoto wa eneo hilo.

Zikiwa zimesalia dakika 21, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or alisherehekea kwa fujo baada ya kuunganisha mpira wa kona uliopigwa na Marcelo Brozovic.

# VAN DIJK ATARAJIA MAKUBWA KWA SLOT

**AMSTERDAM,** UHOLANZI

NYOTA wa Liverpool raia wa Uholanzi wanatarajia kuwasili kwa mwenzao, Arne Slot, katika klabu hiyo kama kocha msimu ujao huku nahodha wao, Virgil van Dijk akijitolea kubakia Anfield.

Van Dijk alisema tayari amezungumza na Slot na kwamba anasubiri kwa hamu msimu unaofuata na kufanya kazi chini ya kocha wa zamani wa Feyenoord ambaye anachukua nafasi ya Jurgen Klopp.

"Bado nina mwaka mmoja kwenye mkataba wangu. Mimi ni nahodha wa klabu na nimeweka wazi kuwa nipo kwa ajili ya kocha mpya na nina shauku katika msimu ujao," alisema Van Dijk wakati Uholanzi ikianza kambi yao ya mazoezi ya kujiandaa na michuano ya Euro 2024.

"Ni wazi, kutakuwa na mabadiliko mengi lakini nina imani tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Nilimpongeza na nimefurahishwa sana naye na familia yake. Tulizungumza kuhusu timu na siku zijazo, lakini sasa mtazamo wangu uko kwenye timu ya taifa."

Mwezi mmoja kabla ya tangazo la Slot na muda mfupi baada ya Klopp kusema kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu, Van Dijk alisema alifikiri kwamba raia mwenzake huyo angefaa sana hapo Anfield.

Ryan Gravenberch alisema Slot amethibitisha thamani yake akiwa Feyenoord, ambapo alishinda ligi ya Uholanzi msimu uliopita.

"Nadhani anaweza kuwa mzuri kwa maisha yangu ya soka, ni kocha ambaye anataka kucheza soka zuri," alisema kiungo huyo mwenye miaka 22, ambaye alisajiliwa kutoka Bayern Munich Agosti mwaka jana.

Slot aliteuliwa kuwa kocha wa Liverpool wiki iliyopita huku Klopp akiondoka baada ya utawala wake wa miaka tisa.

Van Dijk na Gravenberch watamkosa kiungo wao Marten de Roon kwenye michuano ya Ulaya msimu huu baada ya chama cha soka cha Uholanzi kusema katika taarifa Jumatatu kwamba ametolewa nje ya michuano hiyo kutokana na majeraha.

Kiungo huyo wa kati wa Atalanta mwenye umri wa miaka 33 alipata jeraha wiki mbili zilizopita katika fainali ya Coppa Italia, ambayo klabu yake ilipoteza kwa bao 1-0 kutoka kwa Juventus, na hatakuwa fiti kwa wakati kwa ajili ya michuano hiyo nchini Ujerumani.



## Martial aaga rasmi Man United

**MANCHESTER,** ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial ataondoka katika klabu hiyo mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa mwezi Juni, Mfaransa huyo alisema.

Mchezaji huyo mwenye miaka 28 aliwasili Old Trafford akitokea AS Monaco mwaka 2015 na kufunga mabao 90 katika mechi 317 akiwa na Mashetani Wekundu hao wakati akiwa na klabu hiyo.


Kuondoka kulitarajiwa, kwani alikuwa na majeraha katika misimu ya hivi karibuni na hakuwa kwenye kikosi kwa miezi kadhaa.

Martial hakuwa kwenye timu iliyoshinda 2-1 katika fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City Jumamosi.

"Ni kwa hisia kubwa ninawaandikia leo kuwaaga. Baada ya miaka tisa ya ajabu katika klabu, wakati umefika kwangu kufungua ukurasa mpya wa kazi yangu," aliandika kwenye Instagram.

"Mmekuwa msaada usioyumba, katika nyakati nzuri na ngumu. Mapenzi yenu na uaminifu umekuwa chanzo cha mara kwa mara cha motisha kwangu."

Beki Mfaransa Raphael Varane pia alisema ataondoka United mapema mwezi huu, lakinibado hajatoa tamko lolote mpaka sasa.



## Guardiola sasa kutimka Man City

**MANCHESTER,** ENGLAND

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola huenda akaondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu ujao, kwa mujibu wa ripoti.

Guardiola anatarajiwa kuondoka klabuni hapo, kufuatia kugoma kusaini mkataba mpya, baada ya kufanikisha safari ya mafanikio ya kutwaa Ubingwa wa England kwa mara ya nne mfululizo.



Taarifa zilizoripotiwa na Gazeti la The Mail zinaeleza kuwa, uongozi wa Man City ulikuwa kwenye mazungumzo ya kumsainisha mkataba mpya Kocha huyo kutoka nchini Hispania, lakini mpango huo umefifia.

Kutokana na dalili hizo, uongozi wa Man City utalazimika kumsaka Kocha Mkuu mpya mwishoni mwa msimu huu, endapo mazungumzo baina ya pande hizo mbili hayatazaa matunda.

Hadi sasa Guardiola ameiwezesha Man City kutwaa mataji sita kati ya saba ya Ligi Kuu ya England, huku wakishinda

HABARI MICHEZO

# TPBRC YAFUTA PAMBANO LA MWAKINYO NA ALLOTEY

**Na Shufaa Lyimo**

KAMISHENI ya ngumi za kulipwa Tanzania (TPBRC) imesema, haijaidhinisha kufanyika pambano la ngumi kati ya bondia Mtanzania Hassan Mwakinyo dhidi ya Patrick Allotey kutoka Ghana.

Pambano hilo la kimataifa lilipangwa kufanyika Mei 31 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya mpito ya Kamisheni hiyo, Alex Galinoma, alisema wamefanya uamuzi huo kutokana na uvunjaji wa mikataba, ukiukwaji wa vigezo na masharti uliofanywa na mwandaaji wa pambano hilo, Shomari Kimbau kupitia kampuni yake ya 'Golden Boy Promotion Inc', jambo ambalo wamelielezea kuwa linauchafua mchezo huo.

Aidha aliweka wazi kuwa uvunjaji wa vigezo na masharti hayo kuwa ni pamoja uwasilishaji usiokamilika wa nyaraka zinazohitajika, ikiwamo mikataba kamili ya mabondia, rekodi za matibabu na vibali vya tukio hilo.

"Tumeamua kuchukua uamuzi huu wa kutolitambua pambano hilo baada ya kubaini muandaaji wa pambano hilo kutotimiza matakwa ya kufanyika pambano hilo, hajatoa maelezo ya fedha za kuwalipa mabondia pamoja na malipo ya ada ya kufanya pambano hilo," alisema Galinoma.

Aidha, aliongeza kuwa mwandaaji huyo ameshindwa kupata ukumbi unaofaa kufanyika kwa pambano hilo ndani ya muda uliokubaliwa na kuwasilisha nyaraka kuonyesha kupatikana kwa ukumbi huo.

Galinoma, alisema mwandaaji ameshindwa kuwa na mawasiliano na ushirikiano mzuri na tume hiyo kulikopelekea mambo mengi kutokamilika kwa wakati.

Mwandaaji wa pambano hilo, Kimbau hakupatikana kutolea ufafanuzi wa maamuzi hayo licha ya juhudi za kumtafuta.




Katibu Tawala Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Upendo Wella (katikati), akiwa pamoja na wanamichezo wanafunzi wakati akihitimisha kambi ya mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Sekondari Tanzania (UMISETA) kwa mwaka 2024 ngazi ya wilaya. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Lomalisa kutua Azam FC

**Na Shufaa Lyimo**

BEKI wa kushoto wa klabu ya Yanga, Joyce Lomalisa inaelezwa anakaribia kumalizana na klabu ya Azam FC kwa ajili ya kuichezea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Chanzo cha kuaminika kutoka ndani ya uongozi wa Azam FC kimesema mazungumzo baina ya mchezaji huyo yanaendelea vizuri na muda wowote kuanzia sasa watamtangaza mchezaji huyo kuwa mali yao.

"Mazungumzo baina ya Lomalisa na uongozi yamefikia hatua ya nzuri na wanaelekea kuafikiana, naamini wakikubaliana atasaini kwa ajili ya kujiunga na timu yetu msimu ujao," kilisema chanzo hicho.

Alisema Azam msimu ujao imepania kufanya vizuri kwenye mashindano ya ndani na yale ya kimataifa na ndio sababu ya kuboresha kikosi chao.

"Malengo yetu ni kufanya vema msimu ujao, tunaamini usajili tutakaoufanya utaiboresha timu yetu na kushika nafasi za juu," kilisema chanzo hicho.

Lomalisa alikuwa sehemu ya mafanikio ya klabu ya Yanga msimu huu baada ya kuisaidia kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Simba rasmi Shirikisho Afrika, Aziz Ki mfungaji bora Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

ka daraja

Baada ya kukubali kipigo cha mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Azam jana, Geita Gold inaungana na Mtibwa Sugar kushuka daraja moja kwa moja baada ya kumaliza kwenye nafasi ya 15 ikiwa na pointi 25 ambazo hazijaisaidia hata kucheza ‚Play Off'.

JKT, Tabora United kucheza ‚Play Off'

JKT Tanzania baada ya kipigo dhidi ya Simba yenyewe imemaliza katika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 32 na sasa itakwenda kucheza mechi ya mchujo dhidi ya Tabora United, ambayo nayo jana ilikutana na kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Namungo FC kwenye uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Tabora United imemaliza ligi kwenye nafasi ya 14 ikiwa na pointi 27 na kujikuta ikicheza mchezo huo wa Play Off na JKT Tanzania.

Mshindi wa jumla kwenye mchezo huo atakutana na Biashara United iliyoifunga Mbeya Kwanza kwenye michezo miwili ya Play Off kwa timu za ‚Championship', mshindi wa jumla katika mechi hiyo atapata nafasi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Matokeo ya mechi nyingine, Coastal Union iliyomaliza ligi ikiwa nafasi ya nne, ilitoka suluhu dhidi ya KMC nyumbani, hata hivyo imejihakikishia nafasi ya kushiriki Kombe la Shirikisho barani Afrika.

## Rungu kuwashukia wenye imani za kishirikina Ligi Kuu msimu ujao

INATOKA UK. 24

yowasumbua sana msimu huu ni matukio ya imani za kishirikina na wamezipiga sana faini klabu, lakini bado zinaonekana kutowaathiri wahusika.

"Wala isidhaniwe kuwa sisi tunapenda kuwapiga faini ili tupate fedha, sisi faini siyo bajeti yetu ya kujiendesha, lakini tunawajibika kufanya hivyo, naona bado haziwafundishi, tutakuja na sheria nyingine msimu ujao.

Sasa naona tukianza kuwakata pointi labda itasaidia kuondoa vitendo hivi," alisema Mguto.

Msimu uliomalizika jana, kulikuwa na matukio mengi ya vitendo mbalimbali ambavyo kwa mujibu wa bodi hiyo, vilikuwa vinaashiria ushirikina.

Klabu mbalimbali, zikiwamo za Simba na Yanga mara kwa mara zimekuwa zikikutana na adhabu za kutozwa faini.



Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Steven Mguto

Michezo
Jumatano Mei 29, 2024
Nipashe

Ronaldo avunja rekodi Saudia



UKURASA 21

# SIMBA RASMI SHIRIKISHO AFRIKA, AZIZ KI MFUNGAJI BORA LIGI KUU

## ●●● Geita Gold FC yaifuata Mtibwa Sugar, 'Championship', JKT, Tabora United kujiuliza...

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024 imefikia tamati jana na kushuhudia Simba ikiambulia tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kumaliza kwenye nafasi ya tatu ikizidiwa idadi ya magoli na Azam ambao wataungana na Yanga kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hii ni mara ya kwanza baada ya misimu sita kupita ikishiriki Ligi ya Mabingwa Afrika lakini sasa Simba italazimika kushiriki michuano hiyo namba mbili kwa ukubwa Afrika ikiungana na Coastal Union kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano hiyo.

Licha ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya JKT Tanzania kwenye mchezo wa mwisho, Uwanja wa Benjamini Mkapa, matokeo hayo yalizimwa na ushindi wa Azam FC wa mabao 2-0 dhidi ya Geita kwenye uwanja wa Nyankumbu mkoani Geita na kukata tiketi kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya misimu 10 kupita.

Ushindi wa timu hizo umezifanya zote kumaliza msimu kwa kukusanya pointi 69 lakini Azam wakifaidika na uwiano mzuri wa magoli ya kufunga na kufungwa.

Katika mchezo wa jana, Simba ilipata mabao yake kupitia kwa Saido Ntibazonkiza dakika mbili kabla ya mechi kumalizika kwa mkwaju wa penalti, na Willy Onana aliyeingia kipindi cha pili kuandika bao la pili kwenye dakika za nyongeza.

Mkoani Geita, Azam Fc ilipata mabao yake kupitia kwa Yelson Mandoza dakika ya 58 na Feisal Salum ‚Feitoto' dakika ya 71.

Aziz Ki ampiku Feitoto

Licha ya kufunga bao moja kwenye ushindi wa jana, Feitoto alishindwa kutwaa kiatu cha dhahabu cha ufungaji bora baada ya kuzidiwa na kiungo wa Yanga, Azizi Ki ambaye jana wakicheza na Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, alifunga mabao matatu na kuisaidia timu yake kuondoka na ushindi wa mabao 4-1.

Mabao hayo yamemfanya Aziz Ki kufikisha idadi ya mabao 21 akimuacha Feitoto kwa mabao mawili na kuongeza furaha kwa mashabiki wa Yanga ambao mapema wiki iliyopita walishuhudia timu yao ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo.

Mchuano wa kuwania tuzo hiyo ulikuwa mkali na kabla ya michezo ya jana wachezaji wote walikuwa na magoli 18 na hivyo kusubiri michezo ya mwisho kujua nani atakuwa kinara wa mabao msimu huu.

Mabao hayo matatu aliyofunga Aziz Ki yanamfanya kufikisha ‚hat trick' mbili (mabao matatu katika mchezo mmoja) kwenye Ligi Kuu msimu huu ikitanguliwa na ile ya kwanza aliyoipata kwenye mchezo dhidi ya Azam, Oktoba 23, mwaka jana.

Geita Gold yashu-

INAENDELEA UK. 23



**MFUNGAJI BORA 2023/2024**

Kiungo wa Yanga, Aziz Ki ambaye ni mfungaji bora msimu wa 2023/2024 baada ya kufunga mabao matatu kwenye ushindi wa 4-1 dhidi ya Prisons.

## Rungu kuwashukia wenye imani za kishirikina Ligi Kuu msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara imesema kuelekea msimu ujao itatengeneza kanuni ya kuzikata pointi timu zitakazofanya au kuonyesha imani za kishirikina viwanjani wakati wa mchezo. Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Steven Mguto, alisema wao kama bodi, Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na wadau wengine wa soka, wanataka kutengeneza kanuni ya kuzikata pointi timu kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo msimu huu, akisema faini peke yake hazitoshi.

**"Tutaweka sheria kali ambazo klabu zitaogopa na hazitafanya vitu kama hivi vya makusudi, moja ya sheria ni adhabu ya kunyang'anywa pointi, tukiweka hii watu wataatia akili, hawatafanya mambo ya ovyo ovyo," alisema Mguto.**

Amesema moja ya mambo yali-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >